# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

## Kikao cha Saba – Tarehe 8 Septemba, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Waziri wa Kilimo kwa niaba yake Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary – SPS Measures).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa niaba yake Mheshimiwa Khadija Aboud

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Africa Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary – SPS Measures).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Aboud tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 80

### Ufunguzi Rasimi wa Jengo Jipya la Hospitali ya Tunduma

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, ni lini jengo jipya la hospitali lililojengwa Tunduma litafunguliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali

la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kutoa fedha za ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Serikali imeupatia Mkoa wa Songwe kiasi cha shilingi billion 14.8 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali nne kwenye Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Momba na Ileje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeeendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Tunduma ambao mpaka kukamilika inakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 9.5. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza utahusisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* uliogharimu kiasi cha shilingi bilioni nne. Ujenzi wa jengo hilo la ghorofa moja upo kwenye hatua ya umaliziaji. Kuanzia Julai 2021 jengo hilo lilianza kutumika kutoa huduma ya wagonjwa wa nje na kliniki ya mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Tunduma. Ujenzio huo wa majengo yatakayohusishwa ni pamoja na jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la huduma za dharura, jengo la afya ya kinywa na meno, macho, upasuaji na utawala.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza swali la nyongeza

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Sote tunafahamu kwamba ni adhma kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita kumaliza changamoto ya vifo vitokanavyo na uzazi. Pia tunafahamu kwamba kwenye mwaka huu wa fedha Serikali imetenga zaidi ya bilioni 1.5. Lengo ni kuhakikisha kwamba baadhi ya majengo katika Hospitali hii ya Tunduma yanakamilika. Hata hivyo changamoto kubwa ni kwamba mpaka sasa hivi hakuna

jengo la wazazi. Kwa hiyo mimi nilitaka nitoe ombi kwa Serikali, kwamba iangalie sasa namna, kwamba kwenye mwaka huu wa fedha iharakishe kupeleka fedha hizo kwa haraka ili majengo hayo yatakapokamilika yasaidie pia kutoa huduma za uzazi kwa wanawake wa Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; kwa kutambua jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Mbunge wa Jimbo la Tunduma na Naibu Waziri Mheshimiwa David Silinde katika kuhakikisha kwamba hospitali hii inakamilika kwa wakati; nilitaka tu niweze kufahamu na wananchi wa Tunduma, Maporomoko, wa Muungano wa Kaloleni wanataka kumsikia Mbunge wao kwamba anasemaje, kwamba ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa hii hospitali kwa maana ya majengo, vifaa Pamoja na watumishi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali hili nashawishika kumwomba Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI maana sasa umemwita Mbunge, Waziri sasa sijui atajisemea na yeye mwenyewe kwenye jimbo lake. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa wanawake wa Mkoa wa Mkoa wa Songwe, hususan kwenye kupigania masuala yao ya afya, anafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili swali nasema nina *interest* nalo kidogo kwa sababu ni jimbo langu, na bahati nzuri leo nalijibu mimi mwenyewe. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya mama yetu Samia Hassan Suluhu ina dhamira ya dhati kabisa ya kusaidia sekta ya afya nchini. Ndiyo maana katika

bajeti ya mwaka wa fedha huu 2021/2022 katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma imetengewa bilioni 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nimhakikishie tu kama Mbunge wa Jimbo husika fedha hiyo itafika na tutahakikisha kwamba inajenga kama amabvyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba anauliza ni lini hospitali ile itakamilika. Ni kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais imeshatoa fedha awamu ya kwanza imepeleka bilioni nne ambazo zimeshajenga jengo la kwanza na ambalo linatumika sasa hivi. Awamu ya pili tunapeleka bilioni 1.5, kwa hiyo itakuwa imebaki bilioni kama nne ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Serikali ya Awamu ya Sita ina dhamira ya dhati kwenye hilo na ile hospitali itapelekewa fedha zote, kwa sababu muda bado upo na itajengwa na itakamilika kama ambavyo imekusudiwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Kalambo sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Ujenzi wa Kivuko cha Mto Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Mwaka 2015 ya ujenzi wa Kivuko cha Mto Kalambo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege Mbunge wa Jimbo la Kalambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2015 na vilevile ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ya mwaka 2020 ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan umeanza, ambapo upembuzi yakinifu *(Detailed Design)* wa kivuko hicho umekamilika mwaka 2018, ambao ulifanywa na Mhandisi Mshauri *Advanced Engineering Solutions Limited* ya Tanzania kwa kushirikiana na *Teknicon Limited* ya *Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Kivuko hicho chenye urefu wa mita 80 unategemea kugharimu Shilingi Bilioni Nne milioni mia sita themanini na tisa mia saba themanini na tatu elfu mia saba kumi na mbili na senti hamsini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikia sasa ni kwa Serikali kuendelelea kutafuta fedha za ujenzi wa kivuko hicho, pindi fedha zitakapopatikana ujenzi utaanza mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege swali la nyongeza

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba pia nishukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali yanakiri kwamba upembuzi yakinifu ulifanyika mwaka 2018 ambapo aliyekuwa Makamu wa Rais ambaye ndiye Rais wa sasa naye alikuja kutoa ahadi. Swali; natakiwa kuikumbusha mara ngapi Serikali ili ujenzi uanze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni ukweli usiopingika kwamba pale ambapo maeneo yetu na mikoa yetu inapopata fursa ya kutembelewa na viongozi wa kitaifa

kuna mambo ambayo tunanufaika ikiwa ni pamoja na ahadi za viongozi hao wa kitaifa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hawa viongozi wa kitaifa wanapangiwa ziara ili kutembelea mikoa yote ili na sisi tuweze kufaidika katika ahadi ambazo wanatoa viongozi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Silinde majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunakubaliana na mawazo yake Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli Serikali imeshafanya kazi ya awali ya kuandaa *detail design* na imeshakamilika; na kama ambavyo nimemjibu katika swali langu la msingi hapa, nilimwambia kwamba sasa hivi kazi ambayo tunaifanya Serikali ni kutafuta fedha tu ili daraja hilo lianze kujengwa, hicho kivuko ambacho tumekitaja hapo. Kwa hiyo nimwambie tu kwamba hahitaji kuikumbusha Serikali mara kwa mara kwa sababu Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali makini inakumbuka kila ahadi ambayo tumeitoa. Kwa hiyo na kwenye hili nimwondoe shaka kabisa kwamba fedha itakapopatikana tutakamilisha ujenzi huo, na ninaamini ndani ya kipindi hiki cha miaka 5 ya Mheshimiwa Rais wetu tutalitekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linalohusu ziara za viongozi, ninaamini hapa anazungumzia Mawaziri, Naibu Mawaziri, na hususan Ofisi yetu ya Rais TAMISEMI. Nimuahidi tu kwamba nitafika katika eneo lake na tutafanya ziara ya pamoja kwenda kujionea shughuli za kimaendeleo zinazofanyika eneo lile asante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi Mbunge wa Serengeti sasa aulize swali lake

Na. 82

**Kudhibiti Uharibifu Unaofanywa na Wanyamapori – Hifadhi ya Serengeti**

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka na wa kudumu wa kudhibiti wanyamapori katika Hifadhi ya Taifa Serengeti hasa Tembo na Simba ambao wamekuwa wakivamia vijiji na kuharibu mashamba pamoja na kuua watu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini Mheshimiwa Profesa Manya kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii majibu

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K. n. y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori umekuwepo kwa muda mrefu. Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni mwingiliano huo umeongezeka na kusababisha madhara kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuua mifugo na kuharibu mali nyingine za wananchi ikiwemo mazao. Changamoto hii ipo katika maeneo mengi nchini hususan yanayopakana na maeneo yaliyohifadhiwa kama ilivyo kwa Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuwepo kwa changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini, Serikali imeanza kutekeleza

Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Wanyamapori Wakali na Waharibifu. Mpango huo unahusisha yafuatayo.

i. Kutoa mafunzo yatakayowawezesha wanajamii kukabiliana na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu;

ii. Kutoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na wanyamapori hao, na wananchi kuhamasishwa kufuga nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa; na

iii. Kutoa namba maalum za simu *(toll free number)* endapo matukio hayo yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, swali la nyongeza

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu ambayo yametolewa na Serikali. Pengine niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ningemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii akaambatana nami na kutembelea wananchi wa Jimbo la Serengeti kuona ni namna gani tatizo hili ni kubwa na mikakati iliyowekwa, je inaweza kweli kutekelezeka na kumaliza tatizo? Kwa sababu hivi ninavyozungumza kila mara tunapata ripoti za tembo, simba kuvamia wananchi. Pamoja na majibu haya yanayotolewa lakini bado hatuoni tatizo hili likiisha. Kwa hiyo niombe, kwa maana ya kwamba kwa majibu haya Waziri afike na yeye aona kama kweli haya yanaweza yakatosheleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ukitoka katika eneo la mpaka wa hifadhi katika vijiji vingi unaingia kijijini moja kwa moja, hili ni tatizo kubwa sana. Serikali iliwahi kutoa mpango kwamba kutaongezwa *buffer zone* ambayo ni nusu kilomita kuingia ndani ya hifadhi, lakini mpaka leo bado hawajatekeleza. Sasa je, ni lini Serikali itatekeleza uamuzi huu

wa kuongeza *buffer zone* kuingia ndani ya hifadhi ambayo ni moja ya jambo linaloweza likasaidia sana kupunguza mwingiliano huu wa wanyama na makazi ya watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii majibu

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri wake wako tayari kutembelea eneo hilo la Serengeti kama Mheshimiwa Mbunge alivyotaka. Na kwa sababu wako tayari kutembelea eneo hilo. Hata yale majibu yanayohusu *buffer zone* ambayo iliahidiwa napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yatatolewa majibu wakati wa ziara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kassim Hassan Haji Mbunge wa Mwanakwerekwe sasa aulize swali lake.

Na. 83

**Kukamilisha Ujenzi Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe ambacho kiliwekwa jiwe la msingi mwaka 2008 na Kiongozi wa Mbio za Mwenge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Mwanakwerekwe kama ifuatavyo: -

Mheshimwa Naibu Spika, Mwanakwerekwe kuna Kituo cha Polisi cha Daraja "C" ambacho kinatumika hadi sasa na kinafanya kazi kwa saa ishirini na nne, na eneo hilo lilitolewa na Serikali baada ya kuhamisha Idara ya Maonyesho Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo la Magogoni Amani kwa Mabata ndiko kuna jengo la kituo kidogo cha polisi, ambacho kinajengwa kwa nguvu za wananchi na jiwe la msingi liliwekwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka 2008 na ujenzi wake umefikia kwenye hatua ya renta. Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatafuta fedha ili kumalizia ujenzi wa kituo hicho kiweze kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, swali la nyongeza.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza, kituo hiki kina miaka 13 hakijamalizika, je, Waziri atakuwa tayari kuongozana nami kwenda kuzungumza na wananchi wa Jimbo la Mwanakwerekwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, kwa kuwa uhalifu umeongezeka katika Jimbo la Mwanakwerekwe, sasa hivi kuna vibaka na waporaji wengi lakini hata miundombinu ya Serikali nayo imekuwa ikiharibiwa kwa makusudi.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na kadhia hii wanayoipata wananchi wa Jimbo la Mwanakwerekwe?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa wananchi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu rafiki yangu Mheshimiwa Kassim niko tayari kuambatana naye kwenda katika kituo kile na kukiona. Nimuambie kwamba kituo kile nakifahamu na kipo kwa muda mrefu ni kweli, lakini niko tayari kuambatana naye kwenda kukiangalia kituo kile na kuona namna ambavyo tunaweza tukawasaidia wananchi ili kuimarishiwa hizi huduma za ulinzi na usalaama katika eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lingine ni kuhusu vitendo hivi vya uhalifu ambapo vijana wanafanya vitendo vikiwemo vya uvunjifu wa miundombinu na uharibifu wa vitu vingine. Ndani ya jimbo lake kuna kituo kingine kikubwa cha Mwanakwerekwe na hicho kinafanya kazi muda wote, hasa kupitia kituo hiki tutajitahidi tuwe tunafanya doria za mara kwa mara ili kuweza kuwakamata na kuwashughulikia wale wote ambao wanavunja amani ama wanafanya vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine tuko tayari kuendeleza na kuimarisha ulinzi shirikishi ili wananchi na wao waweze kutoa mchango wao katika kulinda amani ya wengine. Kikubwa, tuko tayari kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu wale wote ambao watakuwa wanafanya vitendo hivi. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa Wilaya ya Momba makao yake makuu yako ndani ya Halmashauri ya Momba,

je, ni lini Serikali itatujengea kituo cha polisi ambacho kina hadhi ya wilaya ili kiweze kusaidia kuepusha changamoto na uovu wote ambao unaoendelea ndani ya Jimbo la Momba? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali kupitia Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapatiwa huduma za ulinzi na usalama kupitia kila chombo ambacho wananchi watakuwa wanahitaji. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba awe na Subira, tutajitahidi sana tuhakikishe kwamba ndani ya jimbo hilo au ndani ya eneo hilo ambalo limekosa hicho kituo cha polisi basi tuone namna ya kuweza kupata fedha ili tukawatengenezee wananchi kituo cha polisi waweze kupata huduma za ulinzi. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Chumbuni lina matatizo ambayo yanafanana na Jimbo la Mwanakwerekwe ambalo swali la msingi limeulizwa. Nimekuwa nikiuliza kwa miaka mitano kuhusu Kituo chetu cha Chumbuni ambacho kinahudumia karibu wilaya nzima ya pale mjini, shehia zaidi ya sita, tangu kilikuwa kinafunguliwa asubuhi kinafungwa saa kumi na mbili sasa hivi kimefungwa kabisa. Je, ni lini na sisi tutapata kituo cha polisi kwa sababu kinahudumia zaidi ya shehia sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza, Mbunge wa wawanachi wa Jimbo la Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya vituo tulivifunga kwa sababu nyingi sana. Kuna vituo vingine vilifungwa kwa sababu kubwa tulikuwa na upungufu hasa wa rasilimali watu, kwa maana ya polisi. Nimwambie tu Mheshimiwa kwa kuwa sasa Jeshi la Polisi tumeshatangaza kuajiri askari wapya tutahakikisha kwamba kituo kile tutakifungua na tutapeleka askari ili wananchi waweze kupata huduma za ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi, Mheshimiwa Spika ameshazungumza jambo hilo mara kadhaa. Sasa hivi ukianza na hadithi swali atapewa Mbunge mwingine. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 84

**Benki ya Kilimo Kusaidia Wakulima Wadogowadogo Nchini**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

(a) Je, ni wakulima wangapi wadogo wadogo wamepata mikopo kutoka Benki ya Kilimo ili kukuza tija kwa wakulima hao?

(b) Je, riba za Benki ya Kilimo zinatofauti gani na riba za Benki za Biashara katika kumsaidia mkulima mdogo?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa *Engineer* Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Julai, 2021 Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* imekwishatoa mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 281.74 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kilimo, ufugaji na uvuvi nchini. Mikopo hiyo imewanufaisha wakulima 1,514,695 vikiwemo vyama vya wakulima 151 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utoaji wa mikopo ya moja kwa moja, Benki ya Maendeleo ya Kilimo inasimamia Mfumo wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (*Smallholder Credit Guarantee Scheme – SCGS)* unaolenga kuchagiza mabenki na taasisi za fedha kuongeza ukopeshaji katika sekta ya kilimo. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni 2021, *SCGS* ilitoa udhamini wa mikopo kwa wakulima wadogo 11,244, vikundi vya wakulima 181 na *SMEs* 43 waliopata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 89.92 kutoka benki 9 washiriki katika uendeshaji wa mfuko wa *SCGS*.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa riba, Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* imeweka utaratibu wa kutoza riba kwa kiwango cha asilimia 10 kwa kuzingatia uwezo wa wazalishaji wa madaraja tofauti katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa maana hiyo, mikopo inayotolewa kwa wakulima wadogo hutozwa riba nafuu isiyozidi asilimia 10 na kwa masharti nafuu ya urejeshwaji wake yanayozingatia misimu ya mavuno na mauzo ya mazao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Serikali inaweza kutoa ruzuku ambayo zamani ilikuwa ikitoa kwa wakulima kwa mazao mbalimbali sasa iende kwenye Benki ya Kilimo halafu benki isimamie na kutoa mikopo hiyo kwa riba ndogo sana? Kilimo hakiwezi kukopeshwa zaidi ya asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi karibuni Benki Kuu imetangaza fedha za kusisimua uchumi trilioni moja.

Je, haiwezekani Benki Kuu ikapeleka sehemu ya fedha hiyo kwenye Benki ya Kilimo ili yenyewe isimamie kwa kuwakopesha wakulima kwa riba ndogo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Almas Maige kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ruzuku ya shilingi trilioni 1 ambayo urejeshaji wake utakuwa ni wa riba asilimia 3 ni mkakati maalumu ikiwa ni moja kati ya hatua tano ambazo *BoT* imeziweka kwa ajili ya mabenki yote nchini. Kwa hiyo, *TADB* ni moja kati ya mabenki ambayo yanapaswa kutumia fursa hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TADB* ni miongoni mwa mabenki kadhaa ambayo tayari yameshapeleka maombi hayo kwa ajili ya kupatiwa fedha hizo kwa ajili ya kutekeleza malengo na mikakati yake ikiwemo dhima kubwa ya kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba riba zinapungua kwa kiwango kisichozidi asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna jitihada mbalimbali ambazo kama Serikali inachukua za kuhakikisha kwamba tunaiongezea uwezo *TADB* pamoja na benki nyingine zilizo chini ya mamlaka ya Serikali ili ziweze kupata mitaji ya kutosha pamoja na zenyewe kuwa na utaratibu wa kubuni njia za kujiwezesha kuongeza ukwasi ili waweze kutoa mikopo zaidi na kusaidia sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na sekta nyingine mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki hii ya Kilimo ipo Dar es Salaam lakini wakulima walio wengi wapo katika mikoa mbalimbali kwa maana ya Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Kaskazini na kwingineko. Je, ni lini sasa huduma hizo zitapanuka ili wakulima wote waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Cecilia Paresso amezungumza hoja ya msingi, nimhakikishie kwamba kwa kipindi hiki ambacho *TADB* haijawa na matawi katika maeneo yote nchini imekuwa ikifanya kazi zake kwa utaratibu mzuri wa kuwasaidia wakulima kwa kuweka utaratibu maalumu wa kuratibu kupitia Idara Maalumu ambayo inajihusisha na masuala ya wakulima wadogo wadogo katika benki hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa wazo hili ni jambo jema, nimhakikishie kwamba tumelipokea na tutalifanyia kazi. Pale ambapo hali itaruhusu tutaweza kusambaza huduma ya *TADB* katika maeneo mbalimbali nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 85

**Kiwanda cha Magunia Moshi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. ESTHER E. MALLEKO)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua Kiwanda cha Magunia Moshi Mkoani Kilimanjaro ili kukuza ajira na uchumi kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa **Esther Edwin Malleko,** Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, magunia yanayotokana na zao la mkonge ni moja ya vifungashio muhimu vya mazao ya kilimo hapa nchini. Tanzania ina viwanda nane vinavyoongeza thamani zao la mkonge. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vitatu 3 ni vya kuzalisha magunia ya mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Magunia cha Moshi (*Tanzania Bag Corporation – TBCL)* kilibinafsishwa na Serikali kwa kampuni ya *Mohamed Enterprise Tanzania Limited (METL).* Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali kiwanda hiki kimeshindwa kuzalisha na kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za viwanda vya magunia ya mkonge ni mtambuka na Serikali inazishughulikia kiujumla kwa tasnia yote ya mkonge. Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za utatuzi wa changamoto ikiwemo kulinda wazalishaji wa ndani na kuwatengenezea mazingira bora ya ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa jitihada hizi zinazoendelea zitakuwa ni chachu ya kuinua kilimo cha mkonge na ufufuaji wa viwanda vya magunia ya mkonge kikiwepo kiwanda cha magunia cha Moshi na hivyo kukuza ajira na uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kwenye jibu la msingi Naibu Waziri amesema kwamba magunia ya katani ni ya adimu na yanahitajika sana; na kwa kuwa Mkoani Kilimanjaro ikiwemo Same, Mwanga ni wakulima wazuri wa katani lakini katani hiyo haipati namna ya kuhifadhiwa. Je, ni kwa nini Serikali haioni uharaka sasa kuzungumza na *Mohamed Enterprise* ambaye pia alimiliki mashamba hayo na akamiliki kile kiwanda ili waweze kutengeneza magunia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ametutajia kuwa kuna viwanda nane na vitatu ndiyo vipo *active* lakini magunia haya yanatumika kwenye kuweka kahawa na Mkoa wa Kilimanjaro unalima kahawa na magunia wanaagiza kutoka nje. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo?

**NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa** Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ni kweli kuna changamoto katika zao la mkonge kwa maana ya uchakataji. Sasa hivi Serikali inafanya juhudi kwanza kuongeza uzalishaji wa mkonge kwa maana ya malighafi, lakini pia kuhakikisha wazalishaji kwa maana ya wachakataji kwenye viwanda wanaendelea. Ndiyo maana tumesema moja ya kazi tunazozifanya ni kuwapa vivutio maalumu ikiwemo kuwalinda wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimueleze tu Mheshimiwa Shally Raymond kwamba huyu mwekezaji *METL* kwa maana *Mohamed Enterprise* tayari tumeshaanza kumpa baadhi ya mikataba kwa ajili ya kuzalisha vifungashio kwa maana ya magunia hayo katika zao la korosho. Hii ni mojawapo ya mipango ambayo tunadhani kwa sababu ana uhakika wa soko maana yake atapata mtaji na kuendelea kuzalisha kwenye viwanda hivyo vingine. Kiwanda cha Morogoro tayari kinazalisha tunaamini ataendelea kuzalisha pia katika kiwanda hicho cha Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, kama ambavyo nimesema tumeshaanza kuwapa vivutio maalum ikiwemo kuwapunguzia baadhi ya kodi kwa magunia haya ambayo yanaenda kufanya kazi kwenye vifungashio katika mazao ya kilimo. Kwa hiyo, ameanza na korosho tunaamini akiendelea kuzalisha sasa ataenda kwenye vifungashio kwa ajili ya zao la kahawa na mazao mengine. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Kutoka Msekwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwenye Jimbo la Same Mashariki, Kata ya Ndungu pamoja na Kata ya Mahore kuna mashamba makubwa ya kilimo cha mkonge lakini anayemiliki mashamba hayo haonyeshi kujali zao lile.

Je, Serikali mnasema nini katika hilo?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema moja ya mikakati ya Serikali ni kujihakikishia kuwa tuna malighafi za kutosha ambazo zitaenda kuchakatwa kwenye viwanda vyetu ambavyo tunavihamasisha kuanza kuvifufa sasa.

Kwa hiyo, moja ya mikakati ambayo tumeshaweka kupitia Wizara ya Kilimo ni kuwapa mikakati au kuhakikisha hawa wakulima wanaendeleza sasa haya mashamba ya mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hata hawa wa Same nakuahidi na Wabunge wapo hapa tunaendelea kujadiliana nao lakini kuhakikisha wanaenda kufufua mashamba hayo ili aweze kutoa *raw material* au malighafi kwenye viwanda ambavyo tunaendelea kuvifufua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Vifungashio vya Mafuta ya Mawese**

**MHE. ASSA N. MAKANIKA** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kurekebisha vifungashio vya mafuta ya mawese kwa kuwa wananchi wanaumizwa na kunyonywa kupitia vifungashio vinavyotumika sasa?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo, Mkoa wa Kigoma limeshatengeneza sampuli za vifungashio vya mafuta ya mawese vitakavyotumiwa na wakulima. Kwa kuanzia *SIDO* imetengeneza sampuli za vifungashio hivyo vya lita tano na lita ishirini. Vifungashio hivyo viko katika mfumo wa ndoo ya chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua inayofuata ni sampuli hizo za vifungashio kuwasilishwa kwa Wakala wa Vipimo kwa ajili ya uhakiki wa ujazo huo. Aidha, baada ya Wakala wa Vipimo kuhakiki vifungashio hivyo, itawasilisha sampuli hizo za vifungashio kwa *SIDO* ili viweze kuzalishwa kwa wingi kwa maana ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshatoa maagizo kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* na Wakala wa Vipimo kuharakisha zoezi hilo la urekebishaji wa vifungashio hivyo ili wakulima wa mawese Kigoma wasiendelee

kunyonywa. Aidha, *SIDO* wataanza kuzalisha kwa wingi vifungashio hivyo na kuviuza kwa bei nafuu kwa wazalishaji wa mafuta ya mawese nchini ili kutekeleza kwa vitendo agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, alilolitoa wakati alipokuwa katika ziara yake Mkoani Kigoma mwezi Februari, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, swali la nyongeza.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwanza kwa majibu ya Serikali juu ya zao letu hili la mchikichi ambalo linazaa mafuta ya mawese. Kwa kweli mchikichi ni zao la kipekee sana Kitaifa na Kimataifa, na sisi pia tunategemea tukiona zao hili likiweza kuwanufaisha wananchi wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 19 Desemba, 2020 Mheshimiwa Waziri Mkuu alikaa na wadau wa zao hili pale Kigoma ndani ya Ukumbi wa *NSSF.* Mojawapo ya mambo watu hawa waliomwambia wanahitaji kuona yakifanyiwa kazi ni Bodi ya Mawese na vifungashio maalum.

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Makanika.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua sasa ni nini mkakati wa Serikali ulipofikia katika kutekeleza mambo haya ambayo walimwomba Waziri Mkuu yafanyiwe kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza

la Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, moja ya mikakati ambayo tunatekeleza ni kuanza sasa kutatua changamoto hizo, lakini zaidi tumeshaunda timu ya wataalam baada ya maelekezo ya Waziri Mkuu, wakati huo tumeshaunda timu ya wataalam kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara na Kilimo ambao sasa wataandaa *guidelines* kwa ajili ya vifungashio kwenye mazao haya ya kilimo na bidhaa zake, mazao yote ikiwemo ya mawese.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la bodi, nadhani hili tunalichukua kama moja ya vitu vya kufanyia kazi kama Serikali ili tuweze kuona kama kuwepo kwa Bodi ya Michikichi ni moja ya suluhisho, basi nalo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu wananchi huko wanaumia kama ulivyosema mwenyewe kwenye majibu yako, nafikiri ni muhimu muwe na muda. Maana inaweza ikachukua mwaka mzima hiyo timu inafanya kazi na hiyo bodi nayo, sasa kama mmeshajua tatizo liko wapi basi lifanyieni kazi. Ninyi wenyewe jipeni muda, kwamba ndani ya muda gani mtafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Changamoto ya vifungashio ambayo ipo kwenye mawese ni sawasawa na changamoto ambayo ipo kwenye zao la viazi kule Makete, Mbeya na sehemu nyingine na Serikali ilituahidi.

Je, ni lini vifungashio rasmi vya viazi vitapatikana kwa wananchi wa Makete, Mkoa wa Njombe, Mbeya na sehemu nyingine ili tuondokane na changamoto ya lumbesa ambayo imekuwa ikisumbua kwa muda mrefu hadi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hiyo timu ambayo tumeiunda tumeshawapa *deadline,* kama ambavyo pia umesema, ndani ya mwezi mmoja waje na mkakati au mpango ambao utaweza kutatua changamoto hii. Kama nilivyosema, si kwa zao moja tu la viazi au michikichi na mazao mengine yote. Kwa sababu changamoto ya lumbesa iko katika mazao mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lumbesa ni tatizo pale ambapo inazidi vipimo ambavyo vimekubalika katika zao husika. Kwa mfano katika hali ya kawaida tunasema gunia moja liwe kati ya kilo 95 mpaka 105, kwa hiyo zaidi ya hapo inakuwa ni shida. Sasa inaweza kuwa kifungashio ni kidogo kiasi kwamba ikaonekana kama ni lumbesa lakini kiko ndani ya uzito unaokubalika. Hata hivyo, tunachukua changamoto hizi, kama nilivyosema, Kamati hii itakwenda kuweka sasa mkakati au *guidelines* maalum kwa ajili ya kupata vifungashio *specific* kwa mazao maalum likiwemo hili la viazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kututajia huo muda wa mwezi mmoja. Maana Waziri wa Viwanda na Biashara alishawahi kuja mpaka Mbeya na hadithi ni hiyo hiyo mpaka leo. Sasa nafurahi kusikia kwamba ni mwezi mmoja tutaondokana na hili tatizo ambalo linawanyonya wakulima, lakini pia wafanyabiashara wanapata changamoto kwenye yale maeneo mliyoweka vizuizi kwa ajili ya vipimo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Tathmini ya Mashamba Pori katika Mkoa wa Morogoro**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya mashamba pori yasiyoendelezwa Mkoani Morogoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Julai 2021, jumla ya mashamba 160 yamekaguliwa katika Mkoa wa Morogoro. Kati ya mashamba hayo, mashamba 123 yapo Kilosa, Kilombero (3), Mvomero (13) na Morogoro (21). Aidha, mwezi Aprili, 2021 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan, amebatilisha umiliki wa mashamba 11 yenye ekari 24,159 kutokana na wamiliki wake kukiuka masharti ya umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya utaratibu wa kuyapanga na kuyapima kwa ajili ya matumizi ya wananchi, uwekezaji na ardhi ya akiba na hivi sasa wataalam wanaofanya kazi hiyo wako kwenye maeneo hayo. Kwa sasa Serikali inaendelea na ukaguzi wa mashamba mengine katika Wilaya za Morogoro, mashamba 44 na Mvomero, mashamba 86. Baada ya ukaguzi huo hatua za kisheria zitafuata kwa wamiliki watakaokiuka masharti ya umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ukaguzi na uhakiki wa mashamba katika Mkoa wa Morogoro ni zoezi endelevu likiwa na maslahi

mapana ya Taifa ya kuhakikisha kuwa tunaondoa migogoro inayojitokeza kwa kuwepo mashamba yasiyoendelezwa ipasavyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; ni lini Serikali itatatua mgogoro wa Shamba la Balali lenye ekari 2,000? Kwa sasa shamba lile yapata takribani miaka 20 Balali hajaliendeleza na wananchi wamekuwa wakilima humo. Ni lini sasa Serikali itafuta hati ya Balali na umiliki ule kupewa wananchi wa Jimbo la Mlimba, Kata ya Chita, pale Melela?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini Serikali itatatua mgogoro wa Shamba la Kambenga? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Lukuvi, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba marehemu Balali alikuwa anamiliki, sasa hivi msimamizi wa mirathi ambaye ni mke wake anamiliki shamba hilo alilolisema na nafahamu kwamba halijaendelezwa. Hata hivyo, Serikali ilifanya jitihada za kumtafuta yule mwekezaji na kumpa notisi, akajieleza, lakini bado tulichukua hatua ya kutaka kuchukua sehemu ya shamba hilo ili wananchi waweze kunufaika na yeye kumpa mpango wa muda mfupi aweze kuliendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya wakati wa kupima hilo shamba wananchi hawakuelezwa vizuri, walifikiri

wale wapimaji wanakwenda kumsaidia yule mwenye shamba wakachoma vifaa na magari yaliyokuwa yanatumika kwa kazi ile ya Wilaya ya Kilombero, ni bahati mbaya sana. Kwa hiyo tunachukua hatua nyingine, nimeelekeza kule kwamba sasa tutapeleka notisi ya kumwomba huyu mwenye shamba ajieleze, lakini pia tunafikiria namna ya mwenye shamba kuweza kulipa fidia ya vifaa na mali zilizopotea katika kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili jambo nalifahamu vizuri na nikiwa nje nitamweleza mengine ambayo yalisababisha hili, lakini kwa hapa itoshe tu kwamba Serikali inalitambua na tunachukua hatua juu ya shamba hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; Shamba la Kambenga lilikuwa na mgogoro na vijiji na bahati mbaya sana mkuu wa mkoa aliyepita aliunda timu. Wizara yangu ilitaka kuingilia lakini Mkuu aa Mkoa mpya aliyekuja ameniomba muda kidogo atafsiri ile taarifa ya Kamati aliyoiunda mwenzake. Baada ya taarifa hiyo tutaamua, nilishaamua kumpeleka Kamishna kule, lakini nilisitisha kidogo baada ya maombi ya Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yote haya mawili nayajua, yako ndani ya uwezo wa Wizara. Naomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kukumbushana tutayashughulikia haya yote mawili.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 88

**Kuanzisha Somo Maalum la Maadili na Afya kwa Watoto Kuanzia Shule za Msingi Nchini**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha somo maalum la maadili kuanzia shule za msingi sambamba na somo la afya kwa mtoto ili kukabiliana na mabadiliko ya maumbile ya hisia za mwili pindi mtoto anapoanza kukua ikiwa ni njia ya kukabiliana na tatizo la watoto kuanza kushiriki mapenzi mapema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua umuhimu wa kufundisha maadili kwa mtoto ili kukabiliana na mabadiliko ya maumbile ya hisia za mwili kama njia ya kukabiliana na tatizo la watoto kuanza kushiriki mapenzi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaala ya elimu inayotumika kwa sasa imetilia msisitizo kuhusu masuala ya maadili katika ngazi zote za elimu. Katika ngazi ya elimu ya msingi kuna Somo la Uraia na Maadili ambalo ni somo la lazima kwa wanafunzi wote kuanzia darasa la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, suala la mabadiliko ya maumbile ya mtoto hufundishwa katika Somo la Sayansi na Teknolojia, Stadi za Kazi, na Uraia na Maadili. Katika ngazi ya sekondari masuala ya maadili hufundishwa katika Somo la *Civics* Kidato cha kwanza mpaka cha nne na katika Somo la *General Studies* Kidato cha tano na cha sita. Masomo haya ni ya lazima kwa wanafunzi wote wa sekondari. Aidha, masuala ya afya hufundishwa katika Somo la Biologia ambalo

pia ni somo la lazima kwa wanafunzi wote wa Kidato cha kwanza mpaka cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na zoezi la kuboresha mitaala kwa ngazi za elimu ya awali, msingi na sekondari. Zoezi hilo linahusisha kupokea maoni ya wadau ambayo yatazingatiwa katika maboresho ili kuhakikisha mitaala yetu inakidhi mahitaji na inawajengea wanafunzi maadili ya Kitanzania. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; pamoja na kutoa elimu hii katika shule zetu bado suala la mimba za utotoni ni changamoto katika jamii. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti tunakosea wapi na wakati masomo yote tunatoa kwa watoto wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni kuhusu Uraia. Tuna Somo la Uraia kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha sita, lakini suala la uzalendo limeondoka miongoni mwa wananchi wetu. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka mada maalum ya uzalendo kwenye Somo la Uraia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea

kufanya utafiti na kutilia mkazo juu ya masuala haya ya maadili. Kwa kuliona hilo katika miaka ya nyuma wanafunzi wetu wa shule za msingi walikuwa wanafanya mitihani katika masomo matano, lakini katika mwaka huu katika mitihani ambayo imeanza leo kwa kuona umuhimu wa somo hili la maadili tumeanza sasa kulifanyia mitihani ili kulijengea uwezo na kulititilia msisitizo zaidi. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafanya utafiti na kwa umuhimu wa masomo haya imeonekana ni vyema vilevile nayo yakawa sehemu ya mitihani ya wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, nitoe wito tu kwa ndugu wazazi na walezi; jukumu la malezi ya watoto ni la jamii nzima, siyo la shule wala Walimu peke yake. Hivi sasa imetokea tabia na mtindo kwamba majukumu sasa ya malezi ya watoto wetu yamekuwa ya shule peke yake. Kwa hiyo tutoe wito kwamba, majukumu haya ni ya kwetu kuhakikisha kwamba maadili ya watoto wetu pamoja na mienendo ya taaluma zao tunafuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili, kwamba Serikali sasa tuna mpango gani? Nimtoe wasiwasi vilevile Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, mchakato tunaoendelea nao sasa wa kuboresha mitaala yetu, mambo haya yote tutayatilia mkazo. Waheshimiwa Wabunge mna nafasi nzuri ya kutoa mawazo yenu ili kuweza kuangalia namna gani tunaweza tukatengeneza maadili, lakini tukaweka taaluma vizuri kwa vijana wetu kuhakikisha kwamba tunahitaji kizazi gani chenye maadili gani cha huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. nadhani pia ni muhimu wazazi kufanya sehemu yao, tusiiachie Serikali peke yake kwenye hili zoezi la maadili ya watoto wetu, kwa sababu mambo yote yanaanzia kwenye familia, kwa hiyo kila mtu atimize jukumu lake.

Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali langu la nyongeza kwa Wizara ya Elimu, pamoja na Wizara ya Afya ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma kidogo huko shuleni kulikuwa na utaratibu wa kuwapima mimba wanafunzi kuanzia darasa la sita, la saba na hata sekondari, lakini miaka ya hivi karibuni nimekosa kumbukumbu ni kama suala hilo halipo, kwa sababu na mimi ni mdau wa elimu, labda kama wanapima kwenye shule za Serikali. Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuanza kupima mimba angalau mara mbili kwa mwaka kuanzia darasa la sita, la saba na upande wa sekondari ili kuwaweka wanafunzi wa kike hata wa kiume kuwe na *tension* fulani kwamba kuna kupima mimba mara mbili kwa mwaka na kuacha mimba za utotoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu kimsingi upo pindi watoto wetu wanapotoka likizo tunafanya utaratibu huo. Sasa nimtoe wasiwasi tu Mheshimiwa Mbunge, labda tuweze kuendelea kuutilia tu msisitizo na mkazo ingawa hatuufanyi *in public,* unafanyika kule shuleni na kinakuwa kitu ambacho ni cha kishule zaidi kuliko kutangaza, lakini kimsingi ni utaratibu ambao upo unatumika kwenye shule zetu za Serikali, vijana wetu wanapotoka likizo huwa utaratibu huo unakuwepo. Hata hivyo, tuchukue vilevile wazo lake, tuendelee kuliimarisha na kuliboresha tuweze kuangalia namna gani ya kufanya. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Bugene – Benaco**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ya ujenzi wa Barabara ya Bugene kupitia Pori la Kimisi hadi Benaco kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya Rais ya ujenzi wa barabara ya Bugene kupitia Pori la Kimisi hadi Benaco kwa kiwango cha lami ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bugene – Kasulo – Kumunazi yenye urefu wa kilometa 128.5 ulikamilika mwaka 2019. Taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Bugene – Burigi *Chato National Park* yenye urefu wa kilometa 60 zipo katika hatua ya mwisho kwa kutumia fedha za ndani. Katika mwaka wa fedha huu wa 2021/2022 shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, Serikali imewasilisha Benki ya Maendeleo ya Afrika maombi ya fedha za ujenzi kwa sehemu iliyobaki ya *Burigi Chato National Park* hadi Kumunazi yenye urefu wa kilometa 68.5. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *commitment* ya Serikali, ni lini itajenga hizi kilometa 128.5 za barabara hii kupitia Pori la Kimisi hadi Benaco Ngara kwa kiwango cha lami? Kwa sababu nilishauliza mara nyingi sana ndani ya Bunge hili, najibiwa upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu, sasa naomba *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, Kagera kwamba siyo tena tunaongelea upembuzi yakinifu ama usanifu wa kina. Naomba nimhakikishie kwamba tupo kwenye hatua za manunuzi. Mkandarasi wa barabara hii ameshapatikana na tupo kwenye majadiliano namna ya kuanza hii barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kwamba jinsi anavyofuatilia tutaanza na kilometa 60 kuanzia Bugene kuelekea Kasulo, yaani Benaco. Kwa hiyo, siyo tena habari ya kubabaisha, ni habari ya ukweli kwa sababu tayari tupo kwenye hatua za manunuzi. Kwa hiyo, awe na uhakika kwamba kazi anayofanya kufuatilia, sisi tunafanya na fedha hii tayari imeshatengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara ya Iguguno – Sibiti yenye urefu wa kilometa 102 ina ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Awamu ya Tano: Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuharakisha shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki na Mkoa wa Simiyu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni ahadi ya viongozi wetu na pia ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Singida, Simiyu, Mara na hata Manyara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kati ya barabara ambazo zina barabara nyingi ambapo tayari kwenye bajeti ya mwaka uliopita tumepitisha kuanza kujenga hii barabara kwa sehemu. Ili tuanze kukamilisha hii barabara na katika hili daraja la Simiti, tayari tutakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za maingilio. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Aysharose kwamba Serikali mwaka huu wa fedha kama tulivyoahidi kwenye bajeti na pia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sababu upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tayari umeshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kutokea Msekwa, Mheshimiwa Maimuna Mtanda nadhani ndiyo amevaa kilemba cha *blue* huko.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali kuhusiana na barabara ya kutoka Amkeni – Kitangali hadi Mtama yenye kilometa 74.23 ambayo imeshajengwa kwa lami kwa kilometa 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba *commitment* ya Serikali ni lini itatafuta fedha kutoka kwa wadau wengine wa maendeleo ili barabara kipande kilichobaki kiweze kukamilishwa kwa kiwango cha lami kwa sababu Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo, inajenga kilometa tatu tu kwa mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata jibu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hii barabara aliyoitaja ya Amkeni kwenda Kitangali, tumekuwa tukitenga fedha kidogo kwa ajili ya ujenzi, lakini yote hii ni kutokana na uwezo wa bajeti. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kujenga barabara, siyo hii tu bali ni barabara zote, kwamba kadri fedha inavyopatikana, basi Serikali itaongeza fedha. Ndiyo maana hata tukitangaza barabara pengine kilometa tatu, lakini fedha ikipatikana Serikali hatusiti kuongeza bajeti kwa ajili ya kuendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na barabara hii, kadri fedha itakavyopatikana, Serikali itazidi kuongeza kiasi cha fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao, Mbunge wa Sengerema swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Eric Shigongo.

Na. 90

**Hitaji la Kivuko Kipya – Sengerema**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO K.n.y. MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Jimbo la Sengerema litapata Kivuko kipya angalau kimoja kati ya vivuko vitano ambavyo Serikali imepanga kujenga katika Ziwa Victoria kwa bajeti ya mwaka 2021-2022?

(b) Je, Serikali inafahamu adha ya usafiri wanayoipata wananchi wa Mji Mdogo wa Buyagu Wilayani Sengerema pamoja na wananchi wa Wilaya za Misungwi na Nyang'hwale kwa kukosa chombo madhubuti cha usafiri wa majini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, majibu.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepanga kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini aina na ukubwa wa kivuko kinachohitajika katika eneo hilo. Mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na gharama za kivuko hicho kujulikana, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kivuko kipya katika Jimbo la Sengerema kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea changamoto ya adha ya usafiri iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2021/2022 itatumia wataalam kufanya upembuzi yakinifu katika eneo la Buyagu Wilaya ya Sengerema na Nyang'wale Wilaya ya Misungwi. Upembuzi yakinifu huo utasaidia kubaini aina na ukubwa wa kivuko kinachofaa ili kiwekwe kwenye mpango wa utekelezaji katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Buyagu sasa linaelekea kufikia hatma, lakini bado wananchi wa Kata ya Ilunda Wilayani Sengerema wana adha ya namna hiyo ya kuwa na kivuko kidogo: Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka kivuko kikubwa katika eneo hili la Ilunda? *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa Wilaya ya Sengerema inayo majimbo mawili; lipo Jimbo la Buchosa na Mheshimiwa anafahamu kwamba watu wa Kome, Nyakalilo, Nyakasasa, Mtama wana matatizo makubwa ya usafiri: Je, Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka kivuko kikubwa katika maeneo haya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shigongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika eneo la Sengerema – Buchosa wana bahati kwamba tunajenga

daraja kubwa pale Kigongo – Busisi na kuna vivuko kadhaa vinafanya kazi katika Ziwa Victoria. Baada ya barabara hiyo na daraja kukamilika, maana yake vivuko vile vitahamishwa kwenda maeneo mengine; na maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anataja ndiyo sehemu mojawapo tunaenda kumaliza changamoto hii ili kuweza kutoa huduma katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza sasa tunajenga kivuko kipya ambacho kitafanyakazi Kata Nyakarilo na Kome kitaenda katika eneo hilo. Vile vile tunafanya ukarabati wa kivuko cha MV. SabaSaba ili kiende kusaidia MV2 Kome kuweka huduma katika eneo hilo. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ipo makini sana kupeleka vivuko kwa sababu mbili; moja, ni sehemu ya biashara na pili, ni sehemu ya kutoa huduma. Watupe subira kazi zitakamilika na shida ya usafiri katika eneo hili kwenye visiwa mbalimbali Ziwa Victoria itakuwa imekamilika. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 91

**Kumlipa Mkandarasi wa Barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamlipa Mkandarasi anayetengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Loliondo hadi Mto wa Mbu ili iweze kukamilika na kurahisisha maisha ya Wakazi wa Ngorongoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu sehemu ya Wasso – Sale yenye kilometa 49 ulianza Oktoba, 2017 ambapo hadi kufikia Julai, 2021 utekelezaji wa kazi ulikuwa umefika asilimia 83. Serikali inaendelea kumlipa Mkandarasi wa mradi huu pamoja na Makandarasi wa miradi mingine ya maendeleo inayoendelea hapa nchini kulingana na hati za madai zinazowasilishwa na kuhakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hadi kufikia Juni, 2021, Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii amelipwa jumla ya shilingi bilioni 38.07. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa barabara hii ya kutokea Wasso kwenda Mto wa Mbu ina kilometa 206, lakini kwa miaka minne barabara hii imejengwa kilometa 49 tu; na barabara hii imekuwa inaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Ngorongoro. Hivi juzi tu kuna mama amefia njiani akiwahishwa hospitali kujifungua na tumeona Mheshimiwa Mama Samia akitangaza utalii na barabara hii inahusu utalii. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa mkandarasi huyu anadai shilingi bilioni 21 na walimwongezea muda, alikuwa amalize kujenga barabara hiyo Oktoba, 2019: Je, hamwoni kwamba mnaingiza Serikali katika hasara ya kulipa *penalty? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Catherine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba Mkandarasi anadai shilingi bilioni 21; na anapokuwa amewasilisha hati ya madai, lazima kuna kazi ya kuhakiki madai yao yanafanyika. Kazi hiyo imeshafanyika na Juni mwaka huu 2021, Mkandarasi huyo amelipwa zaidi ya shilingi bilioni 12. Kwa hiyo, mchakato unaendelea, wakikamilisha uhakiki huko Wizara ya Fedha atalipwa fedha ili kazi iweze kuendelea. Mimi mwenyewe nimefika katika barabara hii na nilipata shida kweli barabarani, anachokisema ni kweli, ni barabara ngumu sana, tulipata pancha za kutosha, lakini Serikali imeweka nguvu barabara hii ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, barabara hii ni kweli ina urefu wa kilometa 206, inavyo vipande vinne. Kwa hiyo, tunaanza na hiki cha kwanza; kutoka Wasso kwenda Sale na twende mpaka Mto wa Mbu. Tuna- *engage* vyanzo mbalimbali kupata fedha ili barabara hii iweze kukamilika. Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ni Naibu Waziri wa Serikali hii ya Awamu ya Sita tulikuwa pamoja na anajua tulifanya juhudi kubwa. Tukifanya mpango kumaliza barabara hii, itabadilisha uchumi wa wale watu wa Ngorongoro, itapeleka huduma za kijamii na pia itafungua milango ya watalii na pato la Taifa kwa ujumla wake litaongezeka katika eneo hili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Salma Kikwete.

Na. 92

**Marekebisho ya Sheria ya Ndoa**

**MHE. SALMA R. KIKWETE K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ndoa Bungeni ili kurekebisha Vifungu vya Sheria vinavyohusu Mtoto wa Kike kuolewa akiwa na umri chini ya miaka 18?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali wa yote, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi za ufuatiliaji kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa na kutaka kujua ni lini Muswada huu utawasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa Muswada wa Sheria ya Ndoa ulifikishwa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria mwezi Februari, 2021 kufuatia maamuzi ya Mahakama ya Rufani katika Kesi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi Rebecca Gyumi, Rufaa Na. 204 ya 2017 na Na.5 ya 2016 ya Mahakama Kuu iliyotaka Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho ili mtoto wa kike aolewe akiwa na miaka 18. Kamati baada ya mapitio iliona upo uhitaji wa ushirikishwaji wa wadau wengi zaidi ili kupata maoni zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na zoezi la kushirikisha wadau ambapo hadi sasa Serikali imeweza kufanya mikutano na Viongozi wa Dini katika Mkoa wa Dar es Salaam mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa NaibU Spika, mMkutano wa pili ulifanyika Jijini Dodoma tarehe 2 Julai, 2021 uliojumuisha Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na Viongozi wa Halmashauri ya Mkoa wa Dodoma. Kurejeshwa kwa Muswada huu Serikalini kulitokana na unyeti wa jambo lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali itakapokamilisha michakato iliyoelekezwa na Kamati ya Bunge lako Tukufu, Muswada huu utawasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kisha kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Kutunga Sheria husika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa niaba ya Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, nimeridhika na majibu hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali sasa aulize swali lake.

Na. 93

**Serikali kutafuta Masoko Nje ya Nchi**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, ni lini viongozi wa Kitaifa wataanza kutembelea nchi za nje mahsusi kwa ajili ya kutafuta masoko ya mazao hususan mpunga na mahindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za Viongozi wa Kitaifa nje zimekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, kisiasa na kiuchumi kati ya Tanzania na nchi rafiki. Kutokana na matunda yanayopatikana kupitia ziara za Viongozi wa Kitaifa, Wizara imeendelea kushauri Mamlaka kutembelea nchi za kimkakati kwa kuzingatia maslahi ya Tanzania katika nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu wa Kitaifa tayari wamefanya ziara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na zile za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC).* Ni katika muktadha huo, mwezi Mei, 2021, Wizara iliratibu ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Kenya, ambapo pamoja na mambo mengine alifanikiwa kutanzua, vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha *(NTBs)* vilivyokuwa vikiwakabili wafanyabiashara wakiwemo waliokuwa wakisafirisha mahindi kwenda Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya ni miongoni mwa wanunuzi wakubwa zaidi wa mahindi ya Tanzania kutokana na sifa zake, ubora wake na bei yake nzuri. Hali kadhalika, Wizara pia iliratibu ziara ya Mheshimiwa Rais Samia nchini Burundi, Rwanda na Uganda, ambapo pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais alitumia fursa hiyo kutafuta pia masoko ya bidhaa za mazao kutoka Tanzania ikiwemo mahindi, mpunga na maharage. Aidha, katika ziara ya Burundi, Mheshimiwa Rais aliongozana na ujumbe wa wafanyabiashara ambapo kulifanyika kongamano la biashara kwa lengo la kukuza wigo wa biashara kati ya Tanzania na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na zaidi nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais

kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Hata hivyo, nina swali la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wale mpaka sasa hivi tunavyoongea, bado mazao ya mahindi na mpunga ni mengi sana na kwa kuwa, wanaelekea msimu mpya wa kilimo na bei ya mbolea iko juu na wengine wanashindwa kufanya marejesho ya benki.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba muda umefika sasa wa kuunda *task force* maalum ya Waheshimiwa Mawaziri. Pengine ikijumuisha na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za sekta husika, ili waende mahsusi kutafuta masoko kabla ya msimu mpya wa kilimo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia upatikanaji wa masoko ya bidhaa ikiwemo mchele, na mahindi. Lakini pia, ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwa kuunda hiyo *task* maalum kwa ajili ya kutafuta hayo masoko. Lakini pia ninaomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, juhudi nyingi sana hivi sasa zinachukuliwa na Serikali katika kutafuta masoko ya bidhaa hizo. Hivi sasa ninavyosema kuna timu ya Wizara ya Kilimo ambayo iko nchini Comoro, mahsusi kwa kutafuta soko la bidhaa ya mchele na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni juzi tu, timu hiyo ilitoka *South* Sudan kwa nia hiyo hiyo ya kutafuta soko la mahindi na mpunga na mwisho ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, *TANTRADE* wana utaratibu maalum wa kuwasiliana na Balozi zetu ambazo ziko nje

mahsusi kwa ajili ya kutafuta soko kwa bidhaa za Tanzania ikiwemo za mpunga na mahindi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kutokea Msekwa Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali.

Kwa kuwa tatizo la masoko liko pia katika mazao mbalimbali nchini na kwa kuwa sasa hivi, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuweka kitengo cha kutafuta masoko katika Balozi zetu, ili kiweze kushughulikia tatizo la masoko katika mazao mbalimbali nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tayari Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeunda Idara maalum ya *Economic Diplomacy,* kwa ajili mahsusi ya kutafuta masoko ya bidhaa zetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho linatoka Wizara ya Maji. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 94

**Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Kata Saba za Tarafa ya Chamriho watapatiwa maji kutoka mradi wa maji ya Ziwa Victoria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ni endelevu. Kwa kata saba zilizopo Tarafa ya Chamriho, upatikanaji wa huduma ya maji ni asilimia 61, ambapo vijiji vyote katika Kata tatu za Hunyari, Salama na Nyamuswa vinapata maji kutoka kwenye visima na chemchem.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Kata nne, vijiji ambavyo huduma ya maji siyo ya uhakika ni Mahanga na Mamicheru katika Kata ya Mihingo, Kiroeli, Kambumbu na Nyambuzume Kata ya Nyamanguta, Marambeka na Nyamburumbu Kata ya Ketere na kijiji cha Sanzate Kata ya Mgeta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 mpango wa muda mfupi ni kuboresha huduma ya maji katika vijiji hivyo sita, kupitia utekelezaji wa miradi wa visima virefu ambao utaanza mwezi Oktoba, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali ni kutumia vyanzo vya maji vya uhakika hasa Maziwa makuu. Hivyo, mpango wa muda mrefu ni kufanya upanuzi kutoka miradi mikubwa ya maji inayotumia maji ya Ziwa Victoria.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali nimeyaona lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ulioanza mwaka 2005 ukamalizika mwaka 2018, ambao ulikuwa unatoa maji Ziwa Victoria kuleta Bunda Mjini, na kwa kuwa mradi huo ulikuwa umejumuisha vijiji 30 ambavyo leo tunaviuliza hapa, na kwa kuwa bajeti ya mwaka 2020/2022 imeonyesha kwamba Jimbo la Bunda Vijijini litapewa maji ya Ziwa Victoria kutokea Bunda Mjini. Swali la msingi hapa ni lini sasa Waziri wa Maji ataenda Jimbo la Bunda Vijijini kutangaza mradi huu ambao ameugusia kwenye bajeti ya 2021/2022? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imetumia milioni 40 kufanya utafiti wa vijiji sita ambavyo vina uhaba wa maji kwenye maeneo hayo na maeneo hayo ni Mihingo, Tingirima, Rakana, Jaburundu, Salama A, Kambubu. Serikali imetumia milioni 40 kutengeneza tathmini ya mkakati wa kuchimba na makinga maji kama malambo ya maji hayo. Ni lini sasa itaenda kukamilisha mradi huo ambao uko hapo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Getere kwa ufuatiliaji wa karibu sana na kwa namna ambavyo tumeendelea kushirikiana naye. Nipende kumuambia tu Mheshimiwa Getere kwamba, suala hili la Bunda kuweza kutumia maji ya Ziwa Victoria ni suala ambalo ni la kimkakati Kiwizara na tunafahamu maji yameshafika pale Bunda Mjini na kwa eneo lake la Bunda Vijijini, Serikali ipo katika mkakati wa kuona

kwamba mipango yetu ya muda mrefu inakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na baada ya Bunge hili Wizara itatuma wataalamu pale kwenda kuangalia uwezekano wa kutumia yale maji yaliyofika Bunda Mjini na ikishindikana, basi watafanya *review* mpya kabisa kuona kwamba sasa maji kutoka Ziwa Victoria yanafika Bunda Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na swali lake la pili la kuhusiana na malambo sita ni kweli, Serikali tulipeleka milioni 40 na malambo yale tutakwenda kuyajenga awamu kwa awamu. Tayari lambo la kwanza lipo kwenye utekelezaji asilimia 40 lakini shughuli za ukamilishaji wa lambo hili, utaendelea baada ya mgao ujao wizara kupeleka fedha na kuhakikisha malambo yote sita kila tunavyopata fedha tutapeleka ili yaweze kukamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Mradi wa maji Bunda Mjini ulikuwa wa thamani ya shilingi 10,600,000,000 fedha zilizokwisha kutolewa mpaka sasa ni shilingi 2,600,000,000 bado shilingi bilioni nane. Je, ni lini Serikali itamalizia fedha hizi ili mradi ule uweze kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maboto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mradi ule umeweza kupelekewa fedha hizi shilingi bilioni 2.6 na bado hizo shilingi bilioni 8 na fedha hizi tayari zipo kwenye mpango wa Wizara kuona kwamba tunaendelea kupeleka fedha. Ili kuweza kukamilisha mradi ule na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais

Mama Samia Suluhu Hassan ameendelea kuifanikisha Wizara ya Maji, kwa kuongeza fedha tofauti na namna ambavyo tulipitisha kwenye bajeti yetu. Hivyo, mradi kama huu na wenyewe pia tunaupa jicho la kipekee kabisa kuhakikisha kwamba unakwenda kukamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge lakini pia majibu kutoka kwa Serikali. Ninalo tangazo moja hapa la wageni tulionao Bungeni na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika, walioko *Speaker's Gallery* na hawa wanatoka Kampuni ya Vunja Bei *Group*. *(Makofi)*

Wa kwanza ni Ndugu Fred Ngajiro ambaye ndio anaitwa Vunja Bei na huyu ni Mkurugenzi Mtendaji wa hii Vunja Bei *Group*, karibu sana. Waheshimiwa Wabunge huyu ndio mbunifu na mtengenezaji wa Jezi ya Simba *Sports Club*, karibu sana. *(Makofi)*

Naona watu wanasubiria zisemwe jezi lakini nadhani kwa ujumla wake yeye kama mmojawapo wa vijana wa nchi hii amejitahidi kufanya vizuri. Amejitahidi kuwa mbunifu lakini pia uwekezaji alioufanya ni uwekezaji mkubwa, kwa mtu ambaye ameanza kama mjasiriamali wa kawaida kabisa. Kwa hiyo, tunakupongeza sana Fred Ngajiro kwa kutengeneza ajira lakini kwa hatua mbalimbali unazozichukua. Vijana mbalimbali wanaokuangalia wanajipa moyo kwamba na wao siku moja watakuwa kama wewe na pengine na kuzidi. Tunakupongeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini ameongozana na Ndugu Alphonce Aloyce Shayo ambaye ni Afisa Masoko wa Vunja Bei *Group*, karibu sana. Pia wanaye Ndugu Shabani Alife Abdallah naye ni Afisa Masoko wa Vunja Bei *Group*. Karibuni sana sana sana. *(Makofi/Kicheko)*

Haya Vunja Bei huku unakumbushwa, Ndugu Fred Ngajiro unakumbushwa kwamba kule dukani kule tunatarajia kina dada wapo pia. Kwa hiyo, uwakumbuke na wakina

mama ndio kelele za kina mama humu ndani. Wanatamani kuwaona wakinamama wakiwakilishwa pia.

Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo la wageni wa Mheshimiwa Spika, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary SPS Measures)***

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii sasa nimuite Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda, aje awasilishe Hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kupitisha Azimio la Bunge kuhusu Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya, Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary Measures SPS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Azimio la kuridhia Itifaki ya *East African Community SPS* ni Ibara ya 151 ya Mkataba wa *East African Community* inayoeleza kuwa, nchi wanachama zitaandaa Itifaki katika maeneo yote ya ushirikiano pale inapobidi. Vile vile Ibara za 105 - 110 za Mkataba huo zinataka nchi wanachama kushirikiana katika sekta ya Kilimo na Chakula. Ambapo kwa upande wa viwango vya *SPS* inataka nchi hizo kudhibiti magonjwa ya Mimea na Wanyama, kuianisha sera, Sheria na Kanuni za

kudhibiti visumbufu na magonjwa kuianisha na kuimarisha Taasisi za usimamizi na kuianisha na kuimarisha huduma za ukaguzi na utoaji wa vyeti. Kwa ajili ya usafi wa Mimea *Phytosanitary* na Wanyama au bidhaa za Wanyama *zuo sanitary*. Aidha, Itifaki ya Umoja wa Forodha *(Customs Union)* inataka ushirikiano katika eneo hili ili kukuza biashara ndani na nje ya *East African Community*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi wanachama wa *East African Community* ziliandaa Itifaki ya *SPS* ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 151 ili kuwianisha Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula. Aidha, Itifaki hiyo ilisainiwa na Baraza la Sekta ya Kilimo na Usalama wa Chakula tarehe 12 Julai, 2013 Jijini Arusha na baadaye kuidhinishwa na kuwa nchi wanachama katika Mkutano Mkuu wa 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo iliandaa Waraka wa Mapendekezo ya Kuridhia Itifaki ya *EAC – SPS* kwa kuhusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara mbalimbali zikiwepo Fedha na Mipango, Sheria na Katiba, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mifugo na Uvuvi, Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii na wadau wengine ni Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (*TMDA*), Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania *TOSC*, Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Ukanda wa Kitropiti (*TPRI*), Taasisi Kilele za Mazao ya Bustani (*TARA*), Ofisi ya Hifadhi ya Mimea Zanzibar, Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (*TCCIA*), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka Na. 34/201314 wa mapendekezo ya kuridhia Itifaki ya *EAC - SPS* uliowasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri tarehe 3 Juni, 2015. Ambapo Baraza liliagiza kuwa Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iandae Azimio la Bunge. Kwa ajili ya kuridhia Itifaki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ya

Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary Measures)* na kuliwasilisha Bungeni ili liweze kuridhiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hatua hii ya kuridhiwa kwa Itifaki Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi imefanya majadiliano ya kina kwa kupitia maeneo yote yanayohusu Itifaki kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja na kuainisha mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa utekelezaji ili kulinda na kutetea maslahi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Itifaki yaliyoainishwa katika Ibara ya 2 ni kama ifuatavyo: -

(a) Kukuza biashara ya chakula na bidhaa za kilimo ndani na nje ya jumuiya;

(b) Kuhimiza utekelezaji wa misingi mikuu ya makubaliano ya matumizi ya viwango vya *SPS,* the *WTO agreement on the application of sanitary in phytosanitary measures,* uwianishaji *(harmonization equivalence regionalization transparency)* na tathmini ya athari *(risk assessment)*;

(c) Kuimarisha ushirikiano na uratibu wa viwango na shughuli za afya ya mimea, Wanyama na usalama wa chakula Kitaifa na Kikanda kwa kuzingatia uelewa wa pamoja wa matumizi ya viwango hivyo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(d) Kuimarisha hadhi ya viwango vya *SPS* kwa kuzingatia vigezo vya kisayansi ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki ina Ibara 17, nitataja baadhi ya Ibara hizo na maudhui yake kwa ufupi kama ifutavyo: -

Ibara ya 2, inahusu madhumuni ya Itifaki kama nilivyoeleza katika sehemu ya 3 hapo juu.

Ibara ya 3 inaeleza kuwa mawanda ya ushirikiano ni katika kutumia *adoption* ya viwango vya *SPS* kwa kuwianisha viwango afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula.

Ibara ya 4 hadi Ibara ya 6 zinazungumzia ushirikiano katika masuala yanayohusu afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula na hatua mbalimbali nchi wanachama zinapaswa kutekeleza kupitia ushirikiano huo.

Ibara ya 7 inahusu nchi wanachama kuteua Mamlaka na au Taasisi mahiri *(Competent Authorities)* kwa madhumuni ya Itifaki.

Ibara ya 8 inahusu udhibiti na uwezeshaji wa biashara ya chakula na bidhaa za kilimo kwenye vituo vya mipakani.

Ibara ya 9 inaeleza nchi wananchama zitashirikiana katika kubadilishana taarifa na utaalam kuhusu viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula kupitia uanzishwaji na uendeshaji wa mfumo wa kikanda kuhusiana na madhumuni ya Itifaki.

Ibara ya 10 inahusu ushirikiano katika kutafuta msaada wa kiufundi ili kujenga uwezo wa nchi wanachama katika kutekeleza viwango vya *SPS*.

Ibara ya 11 inahusu nchi wanachama kuwianisha Sera, Sheria, Kanuni na *Program* ili kufanikisha madhumuni ya Itifaki.

Ibara ya 12 inahusu mfumo wa kitaasisi ambapo Baraza la Mawaziri lililoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 9 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye dhamana ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki litaanzisha taasisi zitakazopewa mamlaka ya kutekeleza madhumuni ya Itifaki kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Ibara ya 13 inahusu Mamlaka ya Baraza katika kutunga Kanuni, kutoa maelekezo na kufanya maamuzi kwa kadri inavyoonekana inafaa kwa madhumuni ya Itifaki hii.

Ibara ya 14 inafafanua kwamba usuluhishi wa mgogoro *dispute settlement* kati ya nchi wanachama kuhusu tafsiri au utekelezaji wa Itifaki utatatuliwa kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ibara ya 15 inatoa fursa kwa nchi wanachama kuifanyia marekebisho Itifaki hii kwa kuzingatia Ibara ya 150 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ibara ya 16 inaelekeza kuwa Itifaki itaanza kutumika baada ya kuridhiwa na Nchi zote wanachama wa Jumuiya.

Ibara ya 17 inaeleza kuwa Itifaki hii na Nyaraka zote za kuiridhia zitawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambaye atarejesha nakala kwa Nchi wanachama. Aidha, Itifaki itasajiliwa katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa zenye jukumu la kutekeleza viwango vya *SPS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Ibara ya 16 ya Itifaki, nchi wanachama zinatakiwa kuiridhia Itifaki hii kwa kuzingatia taratibu za nchi husika. Aidha, Ibara ya 17 inataka nchi wanachama zilizoridhia Itifaki kuwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya Maazimo ya Kuridhia Itifaki hii. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepewa Mamlaka ya kuridhia Itifaki hii kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa kuridhia Itifaki hii itaimarisha na kuboresha afya na usafi wa mimea, wanyama na usalama wa chakula. Utekelezaji wa Itifaki hii utaharakisha maendeleo katika sekta ya kilimo, ubora wa mazao, usalama wa chakula na kukua kwa biashara. Baadhi ya matokeo yatakayotokana na kuridhiwa kwa Itifaki hii ni pamoja na:-

(i) Kukua kwa biashara ya chakula na mazao ya kilimo miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya na hivyo kuongezeka kwa fursa ya bidhaa zetu kuingia kwenye soko la Jumuiya bila vikwazo ikiwa ni matokeo ya ulinganifu wa

viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(ii) Itatoa fursa kuimarisha ushirikiano katika kujenga uwezo wa wataalam na utafiti unaolenga viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(iii) Kuwezesha nchi yetu kuwa na nguvu ya pamoja na nchi nyingine katika kutetea bidhaa zinazosafirishwa kutoka ndani ya Jumuiya kuingia katika soko ya Kimataifa.

(iv) Kuimarisha uratibu kwa kuwa na muongozo wa pamoja ndani ya Jumuiya kuhusu afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(v) Kuwepo kwa fursa ya pamoja katika kanda ya kujilinda dhini ya magonjwa na visumbufu vya mimea na wanyama;

(vi) Kuboresha afya na usafi wa mimea, wanyama na usalama wa chakula na hivyo kuimarika kwa maisha ya wananchi katika nchi wanachama;

(vii) Kuongezeka kwa hamasa miongoni mwa wakulima, wafugaji, taasisi na wafanyabiashara ya chakula na mazao ya kilimo katika kuongeza viwango vya ubora wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia misingi ya kitaalam na kisayansi ili kukidhi viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(viii) Kupunguza kwa vikwazo visivyo vya kiforodha mipakani vinavyohusu biashara ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kutokana na uwazi na tathmini ya athari kulingana na makubaliano yanayohusu masuala ya viwango vya afya ya mimea, wanyama na chakula;

(ix) Kuoanisha taratibu za udhibiti na ukaguzi wa mazao mipakani zitakazoondoa matakwa yasiyo ya lazima yanayoambatana na milolongo mirefu ya taratibu; na

(x) Kuimarisha utangamano wa kikanda *regionalization and integration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa utekelezaji wa Itifaki hii, Serikali itahakikisha kuwa:-

(i) Uwiainishaji wa Sera, Sheria na Kanuni kwa mujibu wa Itifaki hii unazingatia maslahi ya Nchi na Jumuiya kwa ujumla ambapo tahadhari dhidi ya uingizaji wa mazao na bidhaa zilizobadilishwa vinasaba *(GMOs)* zitaendelea kuchukuliwa kwa kuzingatia sheria na msimamo wa Tanzania. Aidha, Tanzania itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki haitumiki kama eneo la kuingiza bidhaa na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zinazoweza kuhatarisha usalama wa chakula, usalama wa nchi, wanyama na mazingira.

(ii) Baada ya kuridhiwa kwa Itifaki Serikali itaendelea kuzijengea uwezo taasisi zote zinazohusika na utekelezaji wa Itifaki hii hususan uwezo wa wataalam, utafiti, miundombinu, vifaa na vitendea kazi.

(iii) Mpango wa kutoa elimu utawekwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kama vile redio, runinga, vipeperushi na magazeti. Pia elimu itatolewa kupitia mitandao ya kijamii, uchapishaji wa majalada na tovuti za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo, sasa naomba kuwasilisha Azimio hili kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ifuatavyo:

Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Wanyama na Chakula, *(East African Community Protocol and Sanitary Phytosanitary (SPS) Measures).*

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki, *The East African Community,* kwa Mujibu wa Mkataba ulioianzisha Jumuiya hii ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 30 Novemba, 1999;

NA KWA KUWA, Mkataba huu unazitaka Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushirikiana katika Nyanja mbalimbali ili kuleta maendeleo kwa misingi ya haki, usawa na faida kwa wote;

NA KWA KUWA, Ibara ya 151 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999, imebainisha umuhimu wa Nchi wanachama kuandaa Itifaki zitakazotumika kutoa miongozo ya ushirikiano kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wa Nchi hizo;

NA KWA KUWA, mkataba unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandaliwa itaidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itapaswa kusainiwa na kuridhiwa na nchi wanachama;

NA KWA KUWA, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliandaa Itifaki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ili kutoa muongozo kuhusu viwango vya afya ya mimea, Wanyama na usalama wa chakula;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani, *The World Trade Organization (WTO)* kuanzia tarehe 1 Januari, 1995, hivyo, kutakiwa kutekeleza makubaliano mbalimbali yaliyoridhiwa na wanachama wa shirika hilo na moja ya makubaliano hayo ni kuhusu makubaliano ya utekelezaji wa masuala ya viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula, *WTO Agreement on the Application of Sanitary and Phytosanitary Measures (The SPS Agreement);*

NA KWA KUWA Itifaki ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ilisainiwa na Baraza la Sekta ya Kilimo na Usalama wa Chakula tarehe 12 Julai, 2013 Mjini Arusha na kuidhinishwa katika Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne (14)

wa Wakuu wa Nchi Wanachama kama ilivyoainishwa katika Taarifa ya Kikao cha Tano cha Baraza la Sekta ya Kilimo na Usalama wa Chakula;

NA KWA KUWA madhumuni ya Itifaki kama yaliyovyoainishwa katika Ibara ya 2 ni pamoja na: -

(a) Kukuza biashara ya chakula na bidhaa za kilimo ndani na nje ya Jumuiya;

(b) Kuhimiza utekelezaji wa misingi mikuu ya makubaliano ya matumizi ya viwango vya *SPS (The WTO Agreement on the application of Sanitary and Phytosanitary Measures)* uwianishaji *(harmonization) equivalence regionalization, (transparency)* - uwazi na tathmini ya athari *(risk assessment);*

(c) Kuimarisha ushirikiano na uratibu wa viwango na shughuli za afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula kitaifa na kikanda kwa kuzingatia uelewa wa pamoja wa matumizi ya viwango hivyo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(d) Kuimarisha hadhi ya viwango vya *SPS* kwa kuzingatia vigezo vya kisayansi ndani Jumuiya.

NA KWA KUWA, utekelezaji wa *WTO* wa viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula *WTO agreement on the application of sanitary and phytosanitary measures (The SPS agreement)* unazingatia viwango yaani *SPS standards* vya Mkataba wa Kimataifa wa hifadhi ya mimea *the International Plant Protection Convection (IPPC),* Mkataba wa Afya ya Wanyama (*The World Organization for Animal Health - OIE)* na Mkataba wa Viwango vya Usalama wa Chakula *(The Codex Alimentarius Commission Codex).* Nchi wanachama wa *WTO* zilizopo katika eneo moja na ambazo zina mazingira yanayofanana *(regional conditions)* zinaweza kukubaliana kuweka viwango vya *SPS* kwa ajili ya kulinda afya za walaji na kuzuia kusambaa kwa visumbufu na magonjwa miongoni mwa wanyama na mimea;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo: -

(i) Kukua kwa biashara ya chakula na mazao ya kilimo miongoni mwa Nchi wanachama wa Jumuiya na hivyo kuongezeka kwa fursa ya bidhaa zetu kuingia kwenye soko la Jumuiya bila vikwazo, ikiwa ni matokeo ya ulinganifu wa viwango vya afya ya mimea, Wanyama na usalama wa chakula;

(ii) Itatoa fursa za kuimarisha ushirikiano katika kujenga uwezo wa wataalam na utafiti unaolenga viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(iii) Kuwezesha nchi yetu kuwa nguvu ya pamoja na nchi nyingine katika kutetea bidhaa zitokazo ndani ya Jumuiya kuingia katika soko la Kimataifa;

(iv) Kuimarisha uratibu wa kuwa na mwongozo wa pamoja ndani ya jumuiya kuhusu afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(v) Kuwepo kwa fursa ya pamoja katika Kanda ya kujilinda dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea;

(vi) Kuboresha afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula na hivyo kuimarika kwa maisha ya wananchi katika nchi wanachama;

(vii) Kuongezeka kwa hamasa miongoni mwa wakulima, taasisi na wafanyabiashara wa chakula na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi katika kuongeza viwango vya vya ubora wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia mtazamo wa kitaalam na kisayansi ili kukidhi viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(viii) Kupungua kwa vikwazo visivyo vya kiforodha mipakani vinavyohusu biashara mazao ya kilimo na chakula kutokana na uwazi na tathmini ya athari kulingana na

makubaliano yanayohusu masuala ya viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula;

(ix) Kuoanisha taratibu za uthibiti na ukaguzi wa mazao mpakani zitakazoondoa matakwa yasiyo ya lazima yanayoambatana na milolongo mirefu ya taratibu; na

(x) Kuimarisha utangamano wa Kikanda.

NA KWA KUWA, Itifaki hii haikinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria na Sera za nchi bali inalenga kuimarisha ushirikiano katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na usalama wa chakula baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan kwa kuweka viwango vya *SPS* kulingana na Mkataba wa WTO wa viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula (*WTO Agreement on the Application of Sanitary and Phytosanitary Measures - The SPS Agreement).*

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na kwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na pia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii Bunge hili kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaazimia kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*The East African Community Protocol on sanitary and phytosanitary SPS Measures)* ili kulinda afya na usalama watumiaji wa bidhaa zitokanazo na wanyama na mimea na kuwezesha kukua kwa biashara ya chakula na mazao ya kilimo miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya bila kulazimika kutekeleza masharti ya mkataba ambayo yanaweza kuathiri maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Tutaendelea na utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji aje atoe mawazo ya Kamati, Mheshimiwa Mwenyekiti Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 109(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula yaani *(The East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures)* inatokana na Tanzania kuwa nchi mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization - WTO*) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community – EAC*) iliyoanzishwa mwaka 1999 kupitia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 151 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unazitaka nchi wanachama kushirikiana kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi kupitia miongozo mbalimbali itakayopitishwa na kuridhiwa na nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya Itifaki hii, Ibara ya 105 hadi 110 ya Mkataba unazitaka nchi

wanachama kushirikiana katika masuala ya kilimo, usalama wa chakula na udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama. Vipengele hivyo, vinasisitiza umuhimu wa kuwa na sera zinazofanana katika sekta ya kilimo hususan kwenye maeneo ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu, uzalishaji na usambazaji wa mazao ya mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama, umwagiliaji na utunzaji wa vyanzo vya maji na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba yanayotaka mikataba ya kimataifa ambayo kwa masharti yake inahitaji kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Kwa muktadha huu, tarehe 01 Septemba, 2021 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kushughulikia Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*). Hivyo, taarifa ya Kamati ninayoiwasilisha inatokana na hatua ya Serikali kuwasilisha hoja ya kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula ni utekelezaji wa masharti ya Ibara 151 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madhumuni/ malengo ya itifaki; kwa ujumla itifaki inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge inahusu viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula ina madhumuni ya msingi kama yalivyoainishwa katika kipengele (a) mpaka (j).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa itifaki; maudhui ya Itifaki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula, yamefafanuliwa katika Ibara namba moja mpaka Ibara namba 17 kama zinavyofafanuliwa katika taarifa mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye Ibara tajwa za itifaki, Kamati ilitaka

ufafanuzi kwenye maeneo ya msingi ambayo yalihusu mambo yafuatayo:-

a) Sababu zilizosababisha Tanzania kuchelewa kuridhia itifaki hii tangu ilivyosainiwa na nchi wanachama miaka nane iliyopita ambayo miongoni mwa nchi wanachama ni Tanzania peke yake ndiyo haijaridhia.

b) Kwa kuchelewa kuridhia itifaki hii kumesababisha madhara gani kwa nchi yetu?

c) kwa kuridhia itifaki hii kuna manufaa gani ya moja kwa moja ambayo nchi yetu itapata?

d) Serikali imejiandaa kwa kiasi gani kuanza kutekeleza itifaki hii mara baada ya kuridhia?

e) Je, ni kwa kiasi gani sera na sheria za nchi yetu zimeandaliwa na kurekebishwa ili ziendane na madhumuni ya itifaki husika?

f) Je, ni kwa kiasi gani kamati za kitaifa na mifumo ya kitaasisi imejengewa uwezo na kuimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wabunge.

Aidha, Waziri wa Kilimo ambaye ndiye mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa itifaki hii kwa niaba ya Serikali alieleza Kamati kuwa;

a) Serikali imejiridhisha pasipo shaka kuwa itifaki hii imezingatia maslahi mapana ya Taifa.

b) Nchi yetu ndiyo mnufaika mkubwa wa itifaki hii kutokana na ukweli kwamba Tanzania ndiye mzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na mifugo miongoni mwa nchi wanachama.

c) Tatu, itifaki hii inatoa fursa kwa nchi wanachama kufikia maamuzi ya pamoja na kukubaliana. Aidha, kwa kuzingatia kuwa maamuzi ndani ya jumuiya hufanywa kupitia utayari *(consensus)* wa nchi mwanachama. Hatua hii inaiweka nchi yetu kwenye nafasi nzuri ya kusimamia maslahi mapana ya raia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula, Kamati inakubaliana na dhamira njema ya Itifaki hii miongoni mwa nchi wanachama. Pamoja na dhamira njema iliyopo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

i. Pamoja na kwamba Itifaki hii inawezesha nchi wanachama kuwa na nguvu ya pamoja katika kufanikisha biashara ndani ya Jumuiya kuingia katika soko la Kimataifa; na kwa kutambua ushindani mkubwa wa kibiashara uliopo ni vyema Serikali ihakikishe inajenga uwezo wa ndani wa taasisi zake ili kuziwezesha kushindana kikamilifu, la sivyo tunaweza kuridhia itifaki hii na bado tusifanikishe ipasavyo.

ii. Kwa kuzingatia maudhui yaliyoidhinishwa katika Itifaki hii kwenye Ibara ya 4(2)(b) inayohusu usimamizi wa uingizaji, utafiti na kuendeleza matumizi ya bidhaa za *Living Modified Organisms (GMOs) na Products of Modern Bio-technology and Biological Control Agents*, Kamati inaishauri Serikali mapema iwezekanavyo iharakishe uwepo wa sera, sheria na kanuni zitakazoeleza bayana msimamo wa nchi kuhusu teknolojia ya vinasaba hai kwa mazao ya mimea na mifugo *(GMOs)*.

iii. utokana na muingiliano uliopo katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuhuisha miongozo ya kisera, sheria na kanuni ili iweze kukabiliana na tishio au hatari (*risk*) yoyote itakayoambatana na utekelezaji wa Itifaki hii.

iv. Ili kuweza kunufaika ipasavyo na Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuwaandaa wakulima, wazalishaji na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na mifugo kuzalisha kwa viwango vinavyohitajika ili kuweza kukidhi matakwa ya masoko ya Kimataifa.

v. Pamoja na kuridhia Itifaki hii, Kamati imebaini kuwepo mapungufu ya mifumo ya usimamizi na uwezo mdogo wa Taasisi mbalimbali zinazohusika na afya ya mimea, usalama wa chakula na wanyama. Hivyo ili tuweze kunufaika ipasavyo na Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki kwa kuandaa mpango kazi utakaoainisha namna ambavyo itachukua hatua mbalimbali kuimarisha usimamizi ikiwa ni pamoja na;

a) kuandaa sera mahsusi inayosimamia usalama wa chakula.

b) Kuwa na Sheria mahsusi ya usimamizi wa usalama na ubora wa chakula.

c) Kuimarisha uratibu wa shughuli za usimamizi wa chakula.

d) Kuunda taasisi mahsusi zitakayohusika na usimamizi wa mifumo ya usalama wa vyakula katika sekta mbalimbali.

e) Kubainisha kila jukumu la kila taasisi na kuzipatia uwezo wa kibajeti kwa ajili ya kujiendesha na kufanya tafiti za kisayansi na kuzipatia wataalam kulingana na mahitaji ya mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa na nchi yetu ili kuweza kushindana kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua azimio hili pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama yalivyoorodheshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Profesa Adolf F. Mkenda (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Hussein M. Bashe (Mb), Katibu Mkuu ndugu Andrew M. Massawe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza D. Tumbo pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda na Biashara na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati kamati ilipokuwa ikichambua azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge ndugu Athumani Hussein wa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa namna ya kipekee naishukuru sekretarieti ya Kamati ambao ni ndugu Rachel Nyega na ndugu Virgil Mtui wakisaidiwa na ndugu Waziri Kizingti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili naliliridhie Azimio ya Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA ITIFAKI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KUHUSU VIWANGO VYA AFYA YA MIMEA, WANYAMA NA USALAMA WA CHAKULA (*EAST AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON SANITARY AND PHYTOSANITARY – (SPS) MEASURES*) – KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 109(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*).

Hoja ya kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*) inatokana na Tanzania kuwa nchi mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organizatio - WTO*) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community –EAC*) iliyoanzishwa mwaka 1999 kupitia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 151 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unazitaka nchi wanachama kushirikiana kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi kupitia miongozo mbalimbali itakayopitishwa na kuridhiwa na nchi wanachama.

Kwa madhumuni ya Itifaki hii, Ibara ya 105 hadi 110 vya Mkataba unazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala ya kilimo, usalama wa chakula na udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama. Vipengele hivyo, vinasisitiza umuhimu wa kuwa na sera zinazofanana katika sekta ya kilimo hususan kwenye maeneo ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu, uzalishaji na usambazaji wa mazao

ya mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mimea na wanyama, umwagiliaji na utunzaji wa vyanzo vya maji na usalama wa chakula.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba yanayotaka Mikataba ya Kimataifa ambayo kwa masharti yake inahitaji kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Kwa muktadha huu, tarehe 01 Septemba, 2021 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kushughulikia Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula (*East Africa Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*).

Hivyo, taarifa ya Kamati ninayoiwasilisha inatokana na hatua ya Serikali kuwasilisha Hoja ya Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula ni utekelezaji wa masharti ya Ibara 151 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba.

## 2.0 MADHUMUNI/ MALENGO YA ITIFAKI

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Itifaki inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge inahusu viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula ina madhumuni ya msingi yafuatayo: -

(a) Kukuza na kuimarisha biashara ya chakula na mazao ya kilimo miongoni mwa nchi wanachama ikiwa ni matokeo ya ulinganifu wa viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula;

(b) Kutoa fursa za kuimarisha ushirikiano katika kujenga uwezo wa wataalam na utafiti katika masuala ya viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula;

(c) Kuwezesha nchi wanachama kuwa na nguvu ya pamoja katika kutetea bidhaa zitokazo ndani ya Jumuiya kuingia katika soko la kimataifa;

(d) Kuimarisha uratibu wa masuala ya viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula kwa kuwa na mwongozo wa pamoja ndani ya Jumuiya kuhusu masuala hayo;

(e) Kutoa fursa ya pamoja katika Kanda ya kujilinda dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na wanyama;

(f) Kuboresha afya na usafi wa mimea, wanyama na usalama wa chakula na hivyo kuimarisha kwa maisha ya wananchi katika nchi wanachama;

(g) Kuongeza hamasa miongoni mwa wakulima katika kuongeza viwango vya ubora wa bidhaa kwa kuzingatia mtazamo wa kitaalam na kisayansi ili kukidhi viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula;

(h) Kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha mipakani vinavyohusu biashara ya mazao ya kilimo, wanyama na chakula;

(i) Kuoanisha taratibu za udhibiti na ukaguzi wa mazao mpakani zitakazoondoa matakwa yasiyo ya lazima; na

(j) Kuimarisha utengamano wa kikanda ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## 3.0 UCHAMBUZI WA ITIFAKI

**Mheshimiwa Spika,** Maudhui ya Itifaki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula, yamefafanuliwa katika Ibara ya 17 kama inavyoelezwa hapa chini: -

**Ibara ya 1** inatoa tafsiri ya baadhi ya maneno au misamiati iliyotumika kwenye Ibara mbalimbali za Itifaki kwa madhumuni ya kutoa tafsiri ya maneno na misamiati iliyotumika kwenye Itifaki na kuondoa ukakasi wa kuelewa maana halisi ya ujumbe uliokusudiwa katika maudhui ya Itifaki.

**Ibara ya 2** inabainisha malengo ya Itifaki, kama yalivyoainishwa juu na katika kipengele vya (a) – (d) vya Itifaki,

**Ibara ya 3** inazungumzia mawanda ya matumizi ya Itifaki, kuwa itatumika kukuza ushirikiano katika kuchukua hatua za kudhibiti na kulinda viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula kwa kuhakikisha kuwa nchi wanachama zinakuwa na sera na sheria linganifu kuhusu afya ya mimea, afya ya wanyama na usalama wa chakula.

**Ibara ya 4** inazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala yanayohusu afya ya mimea. Ibara hii inasisitiza: -

i) Umuhimu wa nchi wanachama kuwa na taratibu na miongozo linganifu ya ukaguzi na utoaji wa vyeti vya ubora wa mimea na mazao ya mimea.

ii) Nchi wanachama kuweka taratibu linganifu katika kuratibu uingizaji na utafiti wa zana na pembejeo za kilimo.

iii) Nchi wananchama kuweka miongozo linganifu ya usimamizi na udhibiti wa visumbufu na kuhakikisha usalama wa usafirishaji wa mimea na mazao ya mimea.

iv) Umuhimu wa nchi wanachama kuweka mifumo bora ya udhibiti wa visumbufu na kuweka taratibu linganifu kuhusu utoaji na udhibiti wa nyaraka za uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa mimea. Pia, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuweka taratibu linganifu za utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mimea na mazao ya mimea pamoja na usimamizi wa uingizaji, utafiti na kuendeleza matumizi ya bidhaa za vinasaba hai.

**Ibara ya 5** inazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala yanayohusu afya ya wanyama. Inazitaka pia nchi wanachama: -

i) Kutoa taarifa ya uwepo wa mlipuko wa magonjwa ya wanyama, kuweka taratibu linganifu za ukaguzi, utoaji wa vyeti vya ubora na vibali vya kufanya shughuli za kuzalishia

wanyama, machinjio ya wanyama, uzalishaji wa maziwa na mazao mengine ya wanyama.

ii) Kuweka viwango linganifu vya utunzaji wa vituo vya karantini za wanyama, kuweka utaratibu unaolingana wa utoaji wa vibali vya uingizaji wa wanyama na kuweka mifumo inayolingana ya usajili, utambuzi na ufuatiliaji wa wanyama na mazao ya wanyama.

iii) Kuweka taratibu za udhibiti wa dawa za wanyama na ustawi wa wanyama.

**Ibara ya 6** inahusu usalama wa chakula na umuhimu wa nchi wanachama kushirikiana katika udhibiti wa usalama wa chakula kwa kuweka taratibu zinazolingana za ukaguzi na utoaji wa vyeti vya ubora na vibali, pamoja na kutoa miongozo inayolingana kuhusu udhibiti wa usalama wa chakula na usafirishaji salama wa chakula. Vilevile inazitaka nchi wanachama kuweka masharti yanayolingana ya uingizaji wa chakula na utoaji wa taarifa za uwepo wa vyakula vyenye sumu au hatarishi. Lakini pia kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa usalama wa chakula na kubaini viwango himilivu vya sumu na wadudu wanaoweza kusababisha magonjwa.

**Ibara ya 7** inazitaka nchi wanachama kuwa na chombo au taasisi maalumu kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti masuala ya ubora wa afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula.

**Ibara ya 8** inazitaka nchi wanachama kuweka mazingira yanayowezesha usafirishaji wa chakula na bidhaa za kilimo kufanyika kwa urahisi ndani ya Jumuiya kwa kuainisha na kutangaza vituo vya mipaka vinavyoruhusu usafirishaji wa chakula na bidhaa za kilimo, kufanya ukaguzi wa pamoja na kuruhusu uingizaji wa chakula na bidhaa za kilimo. Vilevile, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kujenga miundombinu na kujenga uwezo wa vituo vya mipakani katika kurahisisha usafirshaji wa chakula na bidhaa za kilimo ndani ya Jumuiya.

**Ibara ya 9** inazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala ya kubadilishana taarifa na uzoefu wa masuala ya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula kwa kuanzisha mifumo ya kuhifadhi taarifa muhimu zinazohusu afya ya mimea, afya ya wanyama na usalama wa chakula.

**Ibara ya 10** inazitaka nchi wanachama kushirikiana katika masuala ya kiufundi kwa ajili kujenga uwezo wa kusimamia miongozo na taratibu za kudhibiti afya ya mimea, afya ya wanyama na usalama wa chakula.

**Ibara ya 11** inazitaka nchi wanachama kuhuisha sera na sheria zao ili kuendana na mahitaji na kufikia malengo yaliyoelezwa katika Itifaki.

**Ibara ya 12** inatoa mamlaka kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzisha na kukasimu madaraka kwa taasisi itakayoona inafaa kusimamia utekelezaji wa masharti ya Itifaki.

**Ibara ya 13** inatoa mamlaka kwa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki kutunga Kanuni, kutoa miongozo na maamuzi yakayowezesha utekelezaji bora wa masharti ya Itifaki hii.

**Ibara ya 14** inaweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro itakayotokana na utekelezaji wa masharti ya Itifaki ambapo inaelezwa kuwa mgogoro wowote baina ya nchi mbili au zaidi kuhusu utekelezaji wa masharti ya Itifaki hii utashughulikiwa kwa mujibu wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 15** inaweka utaratibu wa namna ya kufanya marekebisho ya Itifaki ambapo inaelezwa kuwa Itifaki inaweza kurekebishwa na nchi wanachama kwa kufuata utaratibu uliwekwa na Ibara ya 150 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Ibara ya 16** inaweka masharti ya kuanza kutumika kwa Itifaki. Ibara hii inaeleza kwamba Itifaki itaanza kutumika baada ya

nchi zote kuridhia na kuwasilisha hati ya kuridhia Itifaki hiyo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya.

**Ibara ya 17** inaeleza utaratibu wa kuhifadhi Itifaki na Hati za kuridhia Itifaki. Kwa mujibu wa Ibara hii, Itifaki na Hati za kuridhia Itifaki zitahifadhiwa na Katibu Mkuu wa Jumuiya. Aidha, Ibara hii inampa wajibu Katibu Mkuu wa Jumuiya kutoa nakala zilizothibitishwa za nyaraka hizo kwa kila nchi mwanachama wa Jumuiya.

Vilevile, Katibu Mkuu wa Jumuiya amepewa wajibu wa kusajili Itifaki na Hati za Kuridhia Itifaki kwenye Mashirika yote ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na usimamizi wa utekelezaji wa masuala ya viwango vya afya ya mimea, afya ya wanyama na usalama wa chakula.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye ibara tajwa za Itifaki, Kamati ilitaka ufafanuzi kwenye maeneo ya msingi ambayo yalihusu: -

a) Sababu zilizopelekea Tanzania kuchelewa kuridhia itifaki hii tangu iliposainiwa na nchi wanachama miaka nane (8) iliyopita ambapo miongoni mwa nchi wanachama ni Tanzania peke yake ndio haijaridhia.

b) Je kwa kuchelewa kuridhia Itifaki hii kumepelekea madhara gani kwa nchi yetu?

c) Kwa kuridhia Itifaki hii kuna manufaa gani ya moja kwa moja ambayo nchi yetu itapata?

d) Serikali imejiandaa kwa kiasi gani kuanza kutekeleza itifaki hii mara baada ya kuridhia?

e) Je ni kwa kiasi gani Sera na Sheria za nchi yetu zimeandaliwa na kurekebishwa ili ziendane na madhumuni ya Itifaki husika?

f) Je ni kwa kiasi gani Kamati za Kitaifa na Mifumo ya Kitaasisi imejengewa uwezo na kuimarishwa?

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wabunge. Aidha, Waziri wa Kilimo ambaye ndio mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Itifaki hii kwa niaba ya Serikali aliieleza Kamati kuwa: -

i) Serikali imejiridhisha pasipo shaka kuwa Itifaki hii imezingatia maslahi mapana ya Taifa;

ii) Nchi yetu ndio mnufaika mkubwa wa Itifaki hii kutokana na ukweli kwamba, Tanzania ndio mzalishaji mkubwa wa mazoa ya kilimo na mifugo miongoni mwa nchi wanachama;

iii) Itifaki hii inatoa fursa kwa nchi wanachama kufikia maamuzi ya pamoja na kukubaliana. Aidha, kwa kuzingatia kuwa maamuzi ndani ya Jumuiya hufanywa kupitia utayari (*consensus*) wa nchi mwanachama hatua hii inaiweka nchi yetu kwenye nafasi nzuri ya kusimamia maslahi mapana ya raia wake.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya uchambuzi wa Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula, Kamati inakubaliana na dhamira njema ya Itifaki hii miongoni mwa nchi wanachama. Pamoja na dhamira njema iliyopo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatoa: -

i) Pamoja na kwamba Itifaki hii inawezesha nchi wanachama kuwa na nguvu ya pamoja katika kufanikisha biashara ndani ya Jumuiya kuingia katika soko la Kimataifa. Na kwa kutambua ushindani mkubwa wa kibiashara uliopo ni vyema Serikali ihakikishe inajenga uwezo wa ndani wa Taasisi zake ili kuziwezesha kushindana kikamilifu la sivyo tunaweza kuridhia itifaki hii na bado tusinufaike ipasavyo.

ii) Kwa kuzingatia maudhui yaliyoainishwa katika Itifaki hii kwenye Ibara ya 4(2)(b) inayohusu usimamizi wa uingizaji, utafiti na kuendeleza matumizi ya bidhaa za *Living Modified*

*Organisms(GMOs) na Products of Modern Biotechinology and Biological Control Agents*, Kamati inaishauri Serikali mapema iwezekanavyo iharakishe uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni zitakazoeleza bayana msimamo wa nchi kuhusu teknolojia ya vinasaba hai kwa mazao ya mimea na mifugo (GMOs);

iii) Kutokana na mwingiliano uliopo katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Sekta za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuhuisha miongozo ya Kisera, Sheria na Kanuni ili iweze kukabiliana na tishio au hatari (*risk*) yoyote itakayoambatana na utekelezaji wa Itifaki hii.

iv) Ili kuweza kunufaika ipasavyo na Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mkakati wa makusudi wa kuwaandaa wakulima, wazalishaji na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na mifugo kuzalisha kwa viwango vinavyohitajika ili kuweza kukidhi matakwa ya masoko ya kimataifa.

v) Pamoja na kuridhia Itifaki hii, Kamati imebaini kuwepo mapungufu ya mifumo ya usimamizi na uwezo mdogo wa Taasisi mbalimbali zinazohusika na afya ya mimea, usalama wa chakula na wanyama. Hivyo ili tuweze kunufaika ipasavyo na Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki kwa kuandaa Mpanga Kazi utakaoainisha namna ambavyo itachukua hatua mbalimbali kuimarisha usimamizi ikiwa ni pamoja na;

i) Kuandaa Sera mahususi inayosimamia Usalama wa Chakula;

ii) Kuwa na Sheria mahususi ya Usimamizi wa Usalama na Ubora wa Chakula;

iii) Kuimarisha Uratibu wa Shughuli za Usimamizi wa Chakula;

iv) Kuunda Taasisi mahsusi zitakayohusika na Usimamizi wa Mifumo ya Usalama wa Vyakula katika Sekta mabalimbali;

v) Kubainisha kila jukumu la kila Taasisi na kuzipatia uwezo wa kibajeti kwa ajili ya kujiendesha na kufanya tafiti za

kisayansi na kuzipatia wataalamu kulingana na mahitaji ya mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa nan chi yetu ili kuweza kushindana kimataifa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Azimio hili pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo - Mjumbe
4. Mhe. Prof. Patrick Aloysi Ndakidemi, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Balozi. Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt.Ritta Enespher Kabati, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
9. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Christopher O. Ole Sendeka, Mb - Mjumbe
12. Mhe.Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Jackson Gideon Kiswaga, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb - Mjumbe

21. Mhe. Mohamed Suleman Omari - Mjumbe
22. Mhe. Tumain Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb - Mjumbe
24. Mhe.Furaha Ntengo Matondo, Mb - Mjumbe
25. Mhe.Yahya Ali Khamisi, Mb - Mjumbe
26. Mhe.Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo Mhe. Profesa Aldolf F. Mkenda (Mb), Naibu Waziri Mhe. Hussein M. Bashe, (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Andrew W. Massawe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Siza D. Tumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda na Biashara na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega na Ndg.Virgil Mtui wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na liridhie Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama, na Usalama wa Chakula.

**Mheshimiwa Spika**, ninaunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

DK. Christine G. Ishengoma, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YABUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

08 SEPTEMBA, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Waheshimiwa Wabunge kwa utaratibu wetu, ninayo majina hapa ya wachangiaji kabla hatujaenda kwenye hatua nyingine. Tutaanza na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Dkt. Ritha Enespher Kabatti ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunruhusu na mimi nichangie hoja hii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuunga mkono hoja hii; na kwa kweli Tanzania imechelewa sana karibu miaka nane imepita tangu wenzetu waliposaini Azimio hili na Itifaki hii kusainiwa na viongozi wa nchi zote za Afrika Mashariki ikabakia Tanzania. Tumepewa sasa mpaka mwezi wa 12 mwisho tuwe tumesaini Itifaki hii. Leo, ni siku ambayo tutajitahidi sana katika kupitisha Azimio hili. Naomba Bunge hili lipitishe Azimio hili kwa sababu lina manufaa sana kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida, huwezi kuongea itu ambacho uko nje. Tulipata matatizo, mahindi yetu yalikwama pale mpakana na tumepata taabu kujadili na wenzetu kwa sababu sisi hatujasaini Itifaki. Lakini, Itifaki hii inapendekezwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu, na kwa kweli ni muhimu, na tafadhali, Itifaki hii ina maana kubwa sana kwetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimejipanga kuongelea sehemu mbili. Ibara mbili tu muhimu katika Itifaki hii na ni Ibara ya 6 inayohusu usalama wa chakula na jinsi ya kudhibiti usalama huo hasa udhibiti wa chakula kinachotokana na mazao ya *GMO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia Serikali ikionge mara nyingi kwamba Tanzania haitaki *GMO* lakini hatuna sera hiyo. Sera inayoeleza kwamba Serikali haitaki au sheria

inayosema Serikali haitaki *GMO.* Katika Itifaki hii *GMO* ni sehemu itakayodhibitiwa na Itifaki hii lakini sasa kama sisi huku hatuna *instrument* inayoweza kutusaidia kwenda kujadiliana kule itatupa taabu. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa ije na sheria au sera au kanuni *instrument* bora ya kupeleka kule kwenye usajili wa itifaki hii kwa katibu Mkuu wa Afrika Mashariki ili mazao ya chakula yanayotokana na *Genetic Modified Organisms (GMO's)* yaweze kudhibitiwa kuingia nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara nyingine ambayo ningependa kuiongelea ni ile Ibara ya 17 kuhusu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kutunza na kuhifadhi *certified* ya nyaraka na sheria na Kanuni ambazo Tanzania inaziwasilisha kule. Hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona sababu ya Serikali iliyotoa kwanini kwa miaka nane hatukusaini Itifaki. Sababu kubwa ilikuwa ni kujiandaa, na tumeona maandalizi mazuri sana. Zimetungwa sheria na zimewekwa mamlaka mbali mbali kuhusu usalama wa chakula, mazao ya wanyama pia kuhusu mimea. Upande wa mimea, sheria kadhaa zimewekwa na mpaka mamlaka imewekwa lakini pia upande wa wanyama na mazao yake tumeweka sheria hizo na kuweka vile vile mamlaka au taasisi za kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hizi ndizo *instrument* zinazosemwa katika Azimio na zinasemwa katika *article* ya 17 ya itifaki hii inayosema na naomba noisome, ya kiingereza kifupi tu, mstari mmoja. Inasema *"The Secretary General shall register the protocol with all Regional and International Organizations responsible for the implication of this"* lakini pia inasema, *"this protocol and all instruments of rectified shall be deposited with the Secretary General who shall transmit certified true copies of the protocol and instruments of the rectification to all partner states".*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Serikali sasa ijiandae na *instrument* hizi, vitendea kazi hivi ambavyo vitatusaidia kwenda kujadili kule wakati tunapoona kwamba Serikali sasa imesimama na msimamo wake kwamba jamani

tuli-*rectify*/kukubaliana/ridhia mkataba/Itifaki hii tulikuja na vitu hivi. Hizo ndizo nyaraka muhimu ambazo Serikali inapaswa kuziunganisha nazo wakati wa kupeleka itifaki hii ambayo sisi tumeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuchangia hilo tu. Kuitaka Serikali iwe Imara katika kuandaa nyaraka hizi na *instrument* za kufanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritha Kabatti, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Aloyce Ndakidemi, Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga ajiandae.

**MHE. DKT. RITHA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Kilimo na watendaji wote kwa kuwasilisha Azimio hili ili tuweze kulijadili. Nimpongeze pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kilimo, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati shusha kidogo hicho kisemeo kiwe kinaendana na sehemu ambapo wewe unazungumza ili sauti iweze kutufikia vizuri.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Profesa Mkenda, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha Azimio hili ili tuweze kulijadili na kuchangia hapa Bungeni. Nimpongeze Mwenyekiti wetu wa Kamati na Wajumbe wa Kamati ya Kilimo kwa maoni na ushirikiano wao walioutoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mmojawapo wa wajumbe wa Kamati, kama Kamati tuliweza kukutana na wataalamu mbalimbali ili kuhoji na kujiridhisha. Pia, tuliweza

kupitia na kuchambua na kuona faida na hasara za kupitisha Itifaki hii. Zipo baadhi ya faida tuliona kama kukuza na kuimarisha biashara ya chakula na mazao ya kilimo na mifugo; kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha mipakani; kuongeza hamasa miongoni mwa wakulima katika kuongeza viwango vya ubora wa bidhaa na mengine mengi ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu amewasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uridhiwaji wa Itifaki hii, Kamati ilibaini upungufu katika mifumo ya usimamizi wa taasisi mbalimbali zinazohusika na afya ya mimea. Ni vyema Serikali ikazingatia ushauri uliotolewa na Kamati ili kuondoa upungufu huo. Pia, kuandaa sera mahsusi inayosimamia usalama wa chakula na kuhuisha sheria mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kuhuisha sheria mara kwa mara kwa sababu kuna wakati tulifanya ziara Kanda ya Ziwa na yapo mapungufu ya kisheria ambayo tuliyaona mfano katika Ziwa Viktoria, kulikuwa kuna sheria ambazo zimewekwa kwa ajili ya nchi wanachama lakini tuliona zile sheria kwa upande wetu zilikuwa hazihuishwi mara kwa mara na kusababisha kwamba nchi yetu pamoja na kuwa nchi yetu ndiyo inamiliki eneo kubwa katika Ziwa Viktoria lakini wenzetu walikuwa wanapata faida kutokana na zile sheria ambazo zilikuwa zinawabana wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara iliyokuwa inapatikana ni kwamba wafanyabiashara wengi walifunga viwanda na kwenda kufungua viwanda Uganda na Kenya. Kwa hiyo, ilikuwa inasababisha nchi yetu kukosa viwanda na ajira kwa sababu kufungwa kwa viwanda vijana wetu wengi walikuwa wanakosa ajira. Kwa hiyo, naomba tunaporidhia Itifaki hii Serikali ijipange kuhuisha sheria mara kwa mara na iwe *flexible* ili wenzetu wanapohuisha sheria zao na sisi tuhuishe za kwetu kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii imezingatia maslahi mapana ya Taifa na nchi yetu ikiwa ni mnufaika mkubwa wa

Itifaki hii kutokana na kuwa ndiye mzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na mifugo miongoni mwa nchi wanachama. Pamoja na kuwa tulikaa miaka nane bila kuidhinisha Itifaki hii, sasa imefika wakati muafaka nchi yetu iweze kuidhinisha itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga na Mheshimiwa Janejelly James Ntate ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nikushukuru mno kwa kunipa nafasi ya kuchangia katioka hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ambayo tunaijadili hapa ni makubaliano ambayo yameingiwa kati ya Tanzania na nchi wanachama wenzetu ikiwa na lengo moja kubwa ambalo ni kuhakikisha kwamba tuna-*harmonize* na kutumia sheria, kanuni ambazo zipo ili kumsaidia Mtanzania ashiriki kikamilifu katika biashara mbalimbali ambazo zinafanyika katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ni kitu muhimu na Wizara husika imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwa-*summon* wakatuletea maelezo mengi marefu tu kuanzia Wizara ya Kilimo, Waziri pamoja na wataalamu wake wamejitahidi sana, Waziri wa Mifugo naye alikuja. Tuliiita Wizara ya Mambo ya Nje nao wakaja wakatuelezea mambo ya ki-protokali na Wizara ya Biashara vilevile walikuja. Kwa hiyo, ni kitu muhimu ambacho tunaliomba Bunge kwa umoja wetu tupitishe Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ni muhimu sana na itatusaidia kwa kiasi kikubwa kufanya biashara na wenzetu kama ambavyo Waziri ameeleza. Sisi kama nchi ya Tanzania wote tunakubali kwamba kwa sekta ya kilimo tuko vizuri, tuna

uwanda mpana sana wa kulima na bidhaa zetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ni nyingi ukianzia mahindi, mbogamboga, maua, maparachichi, matunda, kila kitu tunacho hapa. Vilevile ukija upande wa Wanyama, tunao ng'ombe wengi sana kushinda wenzetu, tunao kuku na samaki wengi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mbele ya safari Wabunge wenzangu nawahakikishia tukipitisha Itifaki hii sisi ndio tutakuwa wanufaika wakubwa kuliko hata wenzetu. Kwa hiyo, kwa umoja wetu naomba tukubaliane tuipitishe, ili tuende mbele, pesa ziingie kwenye mifuko ya raia wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambia hivyo kwa sababu sisi kama nchi tumechukua muda mrefu sana kujiandaa kuingia kwenye Itifaki hii. Kwa hiyo, kwa mawasilisho waliyofanya Mawaziri ambao nimewataja tuko tayari kabisa. Niombe tu tuliwa-*grill* sana Mawaziri kuna wakati ambapo tulikuwa hatujajiridhisha na maelezo tulikuwa tunawaambia nendeni mkatuletee ili tujiridhishe tukawa-*convince* Wabunge wenzetu wakubali Itifaki hii na hilo limefanyika. Kwa hiyo, sisi kama wajumbe wa Kamati tumeridhika kabisa na maelezo ambayo yametoka Serikalini kwamba Itifaki hii ni muhimu na nawaomba tena kwa umoja wetu turidhie ili tuende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ambazo zitapatikana kwa kuridhia Itifaki hii ni nyingi sana, wenzangu wameshataja na sipendi kurudia lakini mimi kama Mchaga nizungumzie ile ya biashara. Tukiridhia Itifaki hii biashara yetu itaongezeka vizuri, tutafanya biashara ya uhakika ya mazao, mifugo, samaki na tutapata kipato cha kutosha kabisa. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuko tayari kusema ukweli kwa maelezo ambayo Waziri ametoa. Nitaeleza vitu vichache tu, tayari wamesha-*identify* taasisi nyeti ambazo zitasimamia afya ya mimea ambapo wameshaunda taasisi inayoitwa *Tanzania Plant Health and Pesticide Authority,*

itakuwa inashiriki kikamilifu, tuta-*compete* vizuri na wenzetu wa nchi za jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya ya wanyama kuna taasisi ambazo zipo, mfano *Tanzania Veterinary Laboratory Agency,* hawa wanashughulikia ng'ombe na wanyama wengine. Kuna *TAFIRI* kwenye mambo ya samaki na kwenye usalama wa chakula tuna Shirika letu la *TBS,* wapo tayari kuhakikisha kwamba viwango ambavyo vinahitajika kutekeleza itifaki hii vinatekelezwa vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niseme kwamba sera mbalimbali zipo tayari. Tumemuelekeza Waziri pale ambapo sera hazipo waende *chap* watengeze sera ili tuendane na wenzetu na tuweze kutekeleza Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kuna ushauri ambao pia tuliutoa naomba nirudie; tunaiomba Serikali chondechonde wahakikishe kwamba tunawajengea uwezo wataalamu wetu ambao watashiriki kwenye Itifaki hii. Tuwe na watafiti waliosoma sawasawa watakaokuwa wanashiriki kwenye utekelezaji wa Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tunaomba tuwe na uwekezaji wa kimkakati. Tuwe na maabara ambazo ni *advanced* zinazoweza kupima na kutoa majibu sahihi ambapo hatutakinzana na wenzetu wa nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ule ugonjwa wa kutokuipatia Wizara pesa ya kutosha. Tunaomba kwenye utekelezaji wa Itifaki hii kwa sababu tutakuwa tunashirikiana na nchi nyingine, Serikali itenge pesa za kutosha ili Profesa Mkenda na wenzake wasikwame kwenye kutekeleza Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja kwenye udhibiti wa usalama wa chakula. Zamani tulikuwa na taasisi iliyokuwa inaitwa *TFDA,* haya ni maoni yangu hayajatoka kwenye Kamati; tulii-*dissolve* ile tukawa na *TMDA* na sasa hivi

*TBS* ndiye anayekagua kuanzia ukaguzi wa magari kule Japan mpaka huku, ana kazi nyingi sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ifikirie uwezekano wa kuwa na chombo ambacho kitakuwa kinaangalia usalama wa chakula. Ikiwezekana kwa mfumo mwingine tuwe na *TFA* nyingine ambayo itakuwa inashugulika na masuala ya kudhibiti ubora wa vyakula ambavyo vitakuwa vinauzwa huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Naomba Wabunge wenzangu tu-*support* Azimio hili, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya na Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula, *East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary Measures – EAC SPS* ambalo linalenga Kuwa na viwango ambavyo vitaleta ushindani katika soko la Afrika Mashariki pale ambapo tutakuwa tunapeleka mazao na wanyama wetu kwenye hili soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nchi yetu ya Tanzania imechelewa kwa miaka nane kama ilivyoelezwa tangu mwaka 2013, lakini nafahamu kwamba ilikuwa ni uwoga. Kama nchi tulikuwa hatuko tayari na tulikuwa tuna mashaka kama hizi fursa zitatolewa pengine wenzetu wanaweza kufaidi zaidi kuliko sisi. Hili lilikuwa ni jambo la msingi kwa sababu ukiangalia misingi yetu kama nchi, tumekuwa na mfumo ule wa kiutawala wa kiujamaa, wakati mwingine umekuwa ukijitenga sana na mifumo hii ya kidunia. Tukafikiri kwamba tukiwa sisi peke yetu pengine ndani ya nchi tunaweza tukafanya mambo yetu, lakini ukiangalia mabadiliko yanayoendelea sasa duniani hatuwezi kusimama peke yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukisoma katika Maandiko Matakatifu, katika Kitabu cha Mwanzo 11:6 pale, inazungumzia umoja; anasema, watu hawa ni wamoja, lugha yao ni moja na sasa hili ndilo wanalifanya na hakuna atakayewazuwia. Sasa tukifikiri sisi kama Taifa tunaweza tukasimama peke yetu hiyo haiwezekani. Ni kweli, ukiangalia ki-teknolojia kama Taifa hatuko tayari, wenzetu wamesha-*advance* kwa mambo mengi, lakini sasa tutasubiri mpaka lini? ukiendelea kusubiri baadaye tutafungiwa milango na tukishafungiwa milango inaweza ikawa pengine ni kazi kubwa kuja kuifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naona hili jambo ni la msingi sana, kama nchi tuchukue hatua tuingie. Yale mapungufu ambayo yapo tuchukue hatua ya kuanza kuyatekeleza na kuziba mianya hiyo ili sasa tuingie kwa miguu miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo naliona katika kutekeleza Itifaki hii ni muhimu sana kuhusisha sekta binafsi. Kwa mfano, ukizungumzia habari ya kulima parachichi kule Njombe, Serikali haiko, lakini watu binafsi wanalima na wanauza kwenye masoko ya nje na haya maparachichi yanakubalika. Ukiangalia wakulima kama akina *ASAS* wanatengeneza vyakula vyenye viwango vya kimataifa.

Kwa hiyo, kama tukihusisha sekta binafsi ni rahisi sana kuwakilisha nchi yetu na kuleta ushindani kwenye soko la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimeona kwamba kama tutaingia kwenye Itifaki hii kuna manufaa makubwa; kwanza ushirikiano wa pamoja lakini tunaweza kuteteana kama Jumuiya. Kama tunaamua kuuza bidhaa zetu pengine Ulaya, Marekani, kwa kuwa sasa tuna Itifaki ya pamoja kama nchi moja inapeleka kule inazuiliwa nchi nyingine inaweza ikaitetea. Kwa hiyo, unakuta kwamba tukiungana kwa namna hii inakuwa ni kazi rahisi tutaweza kuendelea kwa Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaweza kufaidishana kati ya nchi na nchi hasa kimaarifa. Kama tunafanya kazi kwa pamoja tukishirikiana na Wakenya na Warundi na Waganda, tukikaa kwa pamoja tuna-*share* ile wanasema maarifa. Kwa hiyo, kama tukijenga maarifa na ufahamu wa pamoja ni rahisi sana kujenga nguvu ya pamoja na tukaweza kufanikiwa kama Jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nishauri kwa kuwa tayari Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani hii Itifaki pia inaweza kuisaidia Tanzania kufanya biashara hata kwenye masoko ya kimataifa. Ukiangalia pia tumeshapitisha mikataba mingine ya kimataifa inayohusiana na usalama wa mimea na wanyama pamoja na mazao. Kama tulishapitisha hii mingine miaka mingi iliyopita hakuna sababu ya kuikataa hii tunakuwa tunajichelewesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nachoomba hii iwe changamoto kwa Taifa, kwamba tuingie, lakini changamoto ambazo tutazikuta huko tukabiliane nazo kwa sababu tukiendelea kuchelewa haitusaidii kama nchi. Tunaweza tukapima matokeo tangu tumeanza kukataa nchi yetu imefika wapi? Tukiangalia kiuchumi tuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawashauri Wabunge wenzangu kwamba tuipitishe Itifaki hii, lakini changamoto tutakazozikuta kule mbele tukabiliane nazo na baadaye tutavuka na tutapata manufaa makubwa katika kuuza bidhaa zetu zinazotokana na mazao ya kilimo katika nchi za Afrika Mashariki lakini pamoja na nchi za nje. Ni kweli kumekuwa kuna mashaka, ukiangalia hii miaka nane iliyopita kulikuwa kuna vipengele viwili ambavyo tumeona vilikuwa vinaleta mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ilikuwa inaonesha kama tukisaini Itifaki hii tutalazimika pia kufuata mikataba mingine ya *EPA* ambayo inazungumzia ulinzi wa kimazingira ambayo ilianzishwa na Marekani. Pia kulikuwa kuna mashaka kuhusiana na mambo ya *GMO* lakini wenzetu wametueleza kwamba hatulazimiki kwenda kutumia hizi

*GMO,* hasa mbegu, kuleta kwenye ardhi yetu. Kwa hiyo, hicho kipengele kimeangaliwa na sisi tumejiridhisha kwamba kama hilo halitakuwa ni kigezo basi tuko tayari kuingia na kuisaidia nchi yetu iweze kupata manufaa ya kibiashara kwanye hili soko la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa hayo machache, niwashauri Wabunge wenzengu kwamba tuunge mkono halafu twende tukakabiliane na changamoto ambazo tunaziona ziko huko mbele. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janejelly James Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arkadius Rahhi na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu anisaidie kwa haya nitakayochangia kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo, Prof. Mkenda, Naibu wake Mheshimiwa Bashe, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa jinsi mlivyotupitisha kwenye Itifaki hii na tukaweza kuelewa. Hata ambao hatukuwa wanasheria mliweza kutubeba vizuri sana na tukaelewa. Nimpongeze pia Mwenyekiti wangu wa Kamati na niungane naye moja kwa moja kuunga mkono maoni yote ya Kamati yaliyowasilishwa mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie kiti chako kuwaomba Wabunge Wabunge lako Tukufu tukubali kuingia kwenye Itifaki hii ya Afya ya Mimea, Wanyama na Mifugo kwa usalama wake. Sababu zinazonifanya niwaombe tukubali ni kwa mustakabali wa Taifa kwa mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia jiografia ya Tanzania tuko katikati ya nchi zote kimpaka lakini Mungu katubariki kwa ardhi yetu yenye rutuba, ardhi ambayo

inaweza ikaotesha kila zao. Ukiangalia kwa Afrika Mashariki sisi ni wakulima wakubwa wa mahindi, mpunga na hili zao la parachichi ambalo limeongezeka ambalo ni dhahabu ya kijani. Sasa bila kuwa na Itifaki ya kulinda mazao yetu tutakuwa tunaibiwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano leo hii maparachichi yetu yananunuliwa Njombe yanapelekwa Kenya yanawekewa *label* yanapelekwa kama ya Wakenya, lakini kama tutakuwa tumejiunga kwenye hii Itifaki tuna uwezo wa kuwaambia na ku-*harmonize* nao kwamba hapana mkinunua kule lazima yaende na *label* ya Tanzania, kwa hiyo Itifaki itakuwa imetusaidia kwa aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna kilimo cha mbogamboga ambapo mikoa yetu yote iliyo mipakani inaweza ikalima mazao hayo mfano, Kigoma, Kagera, Arusha na Kilimanjaro tunaweza tukaotesha mazao ya mbogamboga na kuweza kuyauza kwa nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mazao ya maua vilevile ambayo yanaoteshwa Kilimanjaro na Arusha, ni Mikoa ambayo ipo mpakani ambayo Itifaki hii itatusaidia maua yetu yasiwe yanapelekwa nchi nyingine yanakwenda nchi za Ulaya na Asia yakionekana yametoka kwa nchi hizo kumbe yametoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara ambazo tunaweza kupata bila kuingia kwenye hii Itifaki ni kwa sababu ya kuwa sisi tutakuwa tunatembea peke yetu, lakini hata kwenye kitabu cha Mungu kwenye Amosi 3:3 imesema; watu wawili msipotembea pamoja hamuwezi kupatana. Kwa hiyo hii Itifaki itupeleke basi tukapatane na Afrika Mashariki nzima, tuweze kwenda kwa pamoja, tuweze kutetea mazao yetu, mifugo yetu na uvuvi wetu wa samaki, kwa sababu tumebarikiwa hata sisi ndio tuna Maziwa, Mito na Bahari kwa asilimia kubwa sisi ndio tuna maji mengi hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunavyokuwa hatuko kwenye Itifaki, kwa mfano ukienda Mkoa wa Kagera boti nyingi za Uganda zinakuja kuvua Kagera na kupeleka samaki wetu, lakini kama tungekuwa tumeshajiunga na tuna Itifaki hii tuna uwezo wa kukaa nao mezani na kuongea nao kwamba wasifanye hicho wanachokifanya basi, wavuvi wa kwetu ndio wavue tuuze ndani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe Wabunge wenzangu kwa hizo sababu nilizozitaja tukubaliane kwa pamoja kwenda kwenye Itifaki hii, hata sisi tulikuwa tuna wasiwasi kwa nini imechukua muda mrefu lakini tumeelezwa ni kwamba nchi ilikuwa kwenye kujiridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa majira na wakati huwa yana wakati wake, umefika wakati ambapo Taifa limejiridhisha sasa kwamba tunaweza tukaenda kwenye Itifaki tukiwa tumejiandaa kwa mfano kwenye mimea tayari wamekuja na sheria tatu zitakazotulinda kwenye Itifaki hiyo. Lakini hata kwenye mifugo na uvuvi tumeielekeza Wizara ya Uvuvi na Mifugo, nao waandae sheria sasa zitakazotulinda kwenye Itifaki hii nao wameahidi watazileta haraka sana kwako, ili Bunge lako lizipitie, basi twende kwenye Itifaki hii tukiwa salama kwa kulinda Watanzania na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia hoja hii ya Azimio la Kuridhia Itifaki ya viwango vya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama pamoja na vyakula vya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East African Community Sanitary and Phytosanitary Protocol).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na tumeingia kwenye Jumuiya hii tukakubaliana mikataba, tukasaini mkataba toka mwaka 1999. Kati ya Mikataba hii inataka tushirikiane Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mambo mbalimbali kwa usawa na haki kwa ajili ya manufaa ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kimojawapo ambacho kipo kwenye mikataba hii ni kipengele namba 151 ambacho kinataka Nchi Wanachama kutengeneza Itifaki ya Kuridhia Afya ya Mimea na Usalama wa Wanyama pamoja na chakula na sisi Tanzania tulisha iandaa hii na kuitayarisha toka mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba sisi ni Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki vile vile sisi ni Wanachama wa Shirika la Biashara la Dunia *(World Trade Organization),* sisi kuwa wanachama wa Jumuiya ya *World Trade Organization* imetulazimu vile vile kutekeleza baadhi ya makubaliano ambayo mojawapo ndio hii Itifaki ya Afya ya Mimea na Usalama wa Wanyama pamoja na Usalama wa Chakula, imebidi tutekeleze kwa sababu na sisi ni wanachama ambapo sasa makubaliano haya yanaitwa *The Agreement on the Application of Sanitary and Phytosanitary Protocol*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hizi lengo lake kubwa ni kulinda afya ya mlaji popote pale. Ndio maana sisi sasa tunatekeleza makubaliano mbalimbali ya kimataifa yakiwemo makubaliano ya usalama wa chakula ambayo inaitwa *the Codex Alimentarius Commission* na vilevile ya usalama wa mimea ambayo ni *International Plant Protection Convention* na pamoja na hii ya usalama wa wanyama *World Organization for Animal Health.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa kuingia au kuridhia Itifaki *key* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa vyovyote vile tuna faida mbalimbali ambazo kama Nchi Tanzania tutaweza kuzifuata na moja wapo ni kukua kwa biashara ya mazao, mifugo pamoja na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoona kwamba kijiografia sisi tuko vizuri, sisi ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula. Kwa hiyo kuwa na *document* ya pamoja, Itifaki itatusaidia sisi kuweza kuingia kwenye biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunafahamu kwamba sisi soko letu kubwa la mahindi lilikuwa Kenya lakini hivi karibuni tumeona vizuizi kwamba mahindi yetu walisema yana sumu kuvu. Sasa tungekuwa tayari tuna hii Itifaki inayokubali kiwango gani cha sumu kuvu ambayo tumekubaliana katika Itifaki hii pengine hiki kizuizi kisingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile sisi Tanzania ndio wafugaji wakubwa, ndio tuna mifugo mingi katika nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo moja kwa moja hii inatupa fursa sisi Watanzania, kwamba sasa tunaweza tukaingia kwenye soko la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine kubwa ni kwamba sasa Itifaki hii itatoa hamasa kwa wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na taasisi mbalimbali kwamba sasa wakazalishe kwa viwango vinavyotakiwa ku-*win* biashara hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Kimataifa. Kwa mfano tu, wafugaji wanapaswa kuogesha mifugo yao pamoja na kuwapa chanjo pengine labda ya ugonjwa wa midomo na kwato, kwa sababu hii mara nyingi imekuwa kizuizi ili kwamba mifugo yao pamoja na mazao ya mifugo kama nyama na maziwa iweze kupata soko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nawashauri na Wabunge wenzangu kwa sababu kuna *round table* kuweza ku-*harmonize* mambo fulani kama *GMO* ambayo sisi kwa kisera tulishayakataa, Itifaki hii ipite na tuweze kufanya biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niungane na wenzangu katika kuchangia hoja hii iliyopo mezani ya Azimio lililoletwa katika Bunge lako Tukufu la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Afya ya Mimea, Afya ya Mifugo na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuzipongeza Wizara zote mbili ambazo zimetupa ushirikiano mkubwa katika kuchambua Azimio hili nikimaanisha Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Wizara nyingine ambazo wataalam wake walikuja tulipokuwa tunafanya uchambuzi wa Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameshasema yote kuhusiana na faida za kuridhia Azimio hili, lakini pia nipende kusema kwamba kuna hasara tusiporidhia kwa sababu ni makubaliano ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Moja ya hasara ambayo tungepata tungeweza kutengwa, tungetengwa katika baadhi ya vipengele vya hii Itifaki kwamba kuna wakati tunataka kutetea maslahi ya mazao yetu haya, afya ya mimea, mifugo yetu, usalama wa chakula lakini wanaweza wakasema ninyi hamna haki ya kusema kwa sababu hamkuridhia hili Azimio. Hivyo ili twende pamoja kama tulivyokubali kuwa wanachama ni muhimu wote kama Bunge lako Tukufu turidhie leo Azimio hili ambalo tumeshalitafakari, tumeshalidadavua na tumejiridhisha kwamba kuna faida kubwa katika kuliunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kutoa wito kwamba turidhie Azimio hili, napenda tu kutoa maoni na ushauri kwa Serikali, kwa sababu tumegundua katika kuchambua utekelezaji wa Azimio kwamba kuna maeneo ambayo tuna upungufu mkubwa. Moja ya maeneo ambayo kuna upungufu mkubwa katika kusimamia afya na usafi wa

mazao yanayohusika ikiwemo kilimo au mazao ya mimea na mifugo na usalama wa chakula ni kwenye hii sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna vitendea kazi vingi vimeshatengenezwa nikimaanisha *instrument* za kusimamia utekelezaji wa Azimio hili lakini pia bado tumegundua kwamba mifumo ya kusimamia na uwezo wa Taasisi za Serikali husika zina upungufu. Hivyo napenda kuisihi Serikali iwekeze kwa dhati katika kujengea uwezo hizo taasisi ili tusije tukasaini ili Azimio tukadhani tumeshafaidika maana yake tutapigika kweli kweli kwani wenzetu walisaini siku nyingi na ina maana wamejipanga. Kwa hiyo, nasi tunatakiwa tujipange, tuwe na sera, tuwe na sheria, tuwe na kanuni, ambazo zitatuongoza katika kuhakikisha kwamba tunafaidika ipasavyo tunapokuwa katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende basi kujielekeza kwenye maoni na ushauri ambao ningependa niongezee pale ambapo Kamati imeishia kwa upande wa afya na usafi wa mifugo. Kwa kweli hii sekta ya mifugo ni moja ya sekta ambayo ukiachia kazi iliyoanza kufanywa na Serikali ya Awamu ya Tano na hii ya Sita ilikuwa ni kama imesahaulika. Ili basi tufaidike katika kuingia kwenye hii Itifaki ni vizuri na napendekeza kiundwe chombo mahsusi kama ilivyo katika Wizara ya Maliasili, wana chombo mahsusi, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, tuanzishe Mamlaka ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Mifugo Tanzania au kwa Kiingereza tungeweza kusema Tanzania *Livestock Infrastructure Development Agency* ambayo itakwenda kusimamia mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ingeweza kusimamia masuala ya masoko ya ndani ya nje maana hatuuzi bidhaa yetu ipasavyo katika masoko ya nje kwa sababu havikidhi viwango. Ingesimamia masuala ya usafirishaji, masuala ya minada kuelekea sehemu za kupakia na kupakua mifugo, ingesimamia machinjio, ingesimamia suala la ngozi kwa sababu kuna ngozi nyingi zinatumwa siku hizi hakuna masoko, ingesimamia masuala ya magonjwa, masuala ya chanjo ya mifugo, ingesimamia masuala

mbalimbali pamoja na usimamiaji wa nyanda za malisho, ingekaa na kutengeneza kanuni za kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya wafugaji. Nyanda za mifugo zingeweza kupimwa zingeweza kuwekewa miundombinu ya maji zingeweza kabisa kuwa *gazetted* kama *National Park* zilivyokuwa *gazetted* na tukawa na maeneo ambayo tungeita kwa lugha ya kigeni *disease free zone.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Wilaya yangu ya Longido asilimia 95 ni wafugaji, ni mapori yasiyofaa kwa kilimo, ni maeneo ya wafugaji ambayo yangeweza hata kuchukuliwa yakafanywa *model* ya maeneo mahsusi ya kufuga mifugo na kunenepesha kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki na nchi za nje. Kwa bahati nzuri tuna kiwanda kikubwa kile ambacho wawekezaji wamejenga, moja ya viwanda vikubwa sana hapa nchini vya kuchakata bidhaa za mifugo, lakini mpaka sasa hivi kina-*operate under capacity* kwa sababu hatujajipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Itifaki itakapokuwa imeridhiwa na tukawa bado hatujaweza kuimarisha afya ya mifugo yetu tutaendelea kukosa masoko kwa sababu mifugo itakayopita ni ile ambayo imevuka vile viwango. Hii Itifaki ni ya viwango, *the whole thing is about standards* ya mazao ya mimea, mazao ya mifugo na usalama wa chakula chote tutakachokuwa tunazalisha Tanzania kitakuwa kinapitishwa kwenye hiyo mizania na tusipopita hakuna mahali tutakwenda kama Taifa hata baada ya kusaini Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeshauri Taifa letu baada ya kuridhia hili Azimio, basi sasa tujifunge mikanda tufuatilie kwa makini dhana ya utekelezaji. Kila sekta, kila taasisi husika ikajengewe uwezo, tukawasomeshe wataalam wetu katika kila fani; mambo ya maabara, afya ya mimea, udongo, mambo haya ya magonjwa ya sumu kuvu yanayoshambulia mazao na kutukosesha soko na kuelimisha wananchi wetu jinsi ya kuzalisha, jinsi ya kuhakiki afya na kutafutia masoko ya ndani na ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, napenda kusema naunga mkono hoja hii iliyo mezani na nalisihi Bunge lako Tukufu liridhie ili tuweze kusonga mbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Itifaki hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula. Kwanza kabla ya kuendelea naunga mkono hoja na nafanya hivyo kwa sababu kuna baadhi ya vitu vilivyomo katika Itifaki hii hata kama tulikuwa tunaogopa na hata tungeendelea kuogopa, hatuwezi kuvizuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano *Article* ya nne inazungumzia *framework for managing pests* na tunafahamu kwamba *pests* hawana mipaka, hata nadhani mwaka huu kulikuwa na nzige hawawezi kusema hawa wamesaini au hawa hawajasaini, wata-*cross* na kama hakuna hiyo *management* maana yake ni kwamba tutakuwa hatufanyi jambo lolote la maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mambo ya *cross pollination* ambalo hilo ni la kuliangalia, kwa mfano hata tunapozungumzia kwamba hatutaki *GMO,* lakini kuna nchi ambazo tunapakana na wanalima na wanaweza wakawa wanakubali *GMO,* sasa *cross pollination* pia hatuwezi kuzuia nyuki kuvuka mpaka kwa mfano. Kwa hiyo kuna vitu ambavyo hata kama hatutaki kwa sababu tunapakana na nchi na hatujajenga ukuta au kuzuia kwa namna yoyote ni lazima vile vitu tutavipata tu. Kwa hiyo kwa kusaini hii Itifaki inatoa *room* ya *discussion* ambayo inaweza ikasababisha hayo mambo tukaya-*manage* vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kunufaika sasa na Itifaki hii ambapo ni kweli kwamba sisi ni wazalishaji wa

chakula na sisi tunaotoka kwenye maeneo tunayozalisha chakula kingi kama mahindi na hata sasa hivi wanazungumzia parachichi, kuna mambo ambayo ili tuweze kunufaika ni vizuri Serikali yetu ikajiandaa. Jambo la kwanza ni maabara na vifaa vya kupimia ubora wa hayo mazao kutoka kwenye chanzo chenyewe. Kwa mfano, mtu anaposafirisha mahindi kutoka Iringa, Sumbawanga au Mbeya halafu afike mpakani ndipo aambiwe hayana ubora wa kutosha, itakuwa ni changamoto na inaweza ikawa ni *disaster* kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo wakati tunapokwenda kusaini hii Itifaki, basi zile sehemu zinazohitaji maabara ya kupimia haya mazao ziwe zimeandaliwa ili wakulima waweze kunufaika. Kwa hiyo, maabara kama hizo na hata sasa hivi kwenye kilimo hiki cha parachichi zile maabara za kupima ubora ambapo sasa mtu anapokuwa na hiyo *certificate* tangu kwenye chanzo, kwa sababu mara nyingi *processing* za *certificate* zinaweza zikafanyiwa mahali ambapo sio kwenye chanzo cha hayo mazao. Kwa hiyo *certification* ikifanyika kule itakuwa rahisi zaidi kwenye kuhakikisha kwamba tunanufaika na *protocol* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiishi tu kwenye maabara zenyewe, bali pia kuwajengea uwezo wakulima kuelewa viwango, kwa sababu wafanyabiashara wapo lakini wengi hawaelewi hivi viwango. Nilifanya utafiti kidogo, kwa mfano, maandalizi yapo ya kutosha sana kwenye sekta ya chakula *TBS* imesha-*harmonize* karibu kila kitu kwenye *East Africa,* kama ni vyakula vilivyobaki basi ni vichache sana. Hata hivyo, pamoja na hiyo *harmonization* ambayo imeshafanyika, ni wakulima au wafanyabiashara wangapi wanajua au labda kuna haja ya kutengeneza *manual* ya *standards* hasa kwa vile vyakula ambavyo tuna-*export* sana na zikawepo kwenye sehemu ambazo watu wanaweza kuzi-*access,* tena zikatengenezwa kwa lugha rahisi ili kila mtu aweze kuelewa *standard* zetu ni zipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivi kwa sababu, kwa mfano *TBS* waki-*harmonize* na ziko pale *TBS*

kwenyewe na wakulima hawaelewi, bado watataka ku-*export* kitu ambacho kinaweza kisiwe *competitive* au kikawa haki-*fit* kwenye hii *protocol.* Hiyo inaweza ikawa ni changamoto ambayo inaweza ikasababisha hii *protocol* ikatupa *disadvantage* badala ya *advantage* kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo napenda pia liangaliwe kwamba kuna elimu kiasi gani ili tuweze kunufaika? Maana yake hofu hii inaweza ikawa hatukujiandaa, sasa tumejiandaa: Je, wananchi wa kule Iringa, Mbeya na Sumbawanga, wanaelewa maandalizi tuliyoyafanya ili waweze ku-*export?* Kwa sababu kweli sisi ni *beneficiary* wakubwa sana wa hii, lakini kama kutakuwa na maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa kweli ni vizuri sana kuiomba hata Serikali kuangalia, kwa sababu kama tunaendelea kuzungumza kwamba kilimo ni uti wa mgongo na ufugaji ni uti wa mgongo pia, lakini kama tusipotengeneza mazingira ya ku-*export* tukabakia kula wenyewe, maana yake ni kwamba haitawezekana kuweza kunufaika na baadhi ya *protocol* ambazo zinatufanya tuweze kufaidika zaidi. Hiyo hofu inaweza ikawa ilikuwa inatokana tu na kutokuelimisha watu ambao wanaweza wakafanya biashara vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa tu kukizungumzia cha mwisho ni huu urahisi wa hizi *certification* wakati wa kusafirisha haya mazao. Kwa sababu inazungumzia, wakati unapotaka kusafirisha upate wapi vibali vya kusafirishia. Sasa kuna mlolongo wa vibali kwenye nchi mbalimbali, hata kwenye nchi yetu unakuta kunakuwa na mlolongo wa vibali vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tuweke *one stop center* ya *certification* ili mtu anapokwenda awe na *one stop center* ya *certification.* Anataka ku-*export,* haya hiyo *Phytosanitary Certificate* aipate pale pale ambapo ambapo anapata kibali cha ku-*export,* aipate pale pale

ambapo anapatia leseni, hizi tunazozungumza hizi *center* ambazo ni sehemu moja na hizi za *Phytosanitary* ziwepo hapo ambapo tayari tumeshaanza kurahisisha. Isije ikawa tunatengeneza hii kikawa kikwazo sasa; mtu amefika kwenye *One Stop Center* anapata vibali vyote, anaambiwa sasa *Phytosanitary* huna, *Sanitary Certificate* huna, hiyo katafute Wizara ya Kilimo.

Kwa hiyo, ku-*merge* kwa sababu hiki ni kitu kipya, kuna *importance* ya ku-*merge* hiyo ili ije isababishe sasa ule urahisi uwepo. Pale palipowekwa zile *One Stop Center; TRA*, sijui nani, wote wale, naye awepo. Kama kuna haja ya kuangalia *document* mahali, iwe rahisi zaidi ili hii isije ikazalishwa kuwa *barrier.* Tusaini halafu baadaye iwe *barrier* wakati wa *implementation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhani, ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye itifaki hii. Kwanza nawapongeza Serikali kwa kuona sasa ni wakati umefika wa kuweza kutuletea azimio hili au itifaki hii. Itifaki hii ina maslahi mapana sana na wakulima wetu pamoja na wafugaji. Pale wafugaji na wakulima wanaponufaika ni moja kwa moja Taifa letu linakwenda kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kwenye mambo kadhaa ili tuweze kufanya vizuri. La kwanza, kwenye itifaki hii, kwenye suala zima la mifugo, afya ya mimea pamoja na mazao yote, tuna upungufu mkubwa wa wagani ambao wao ndio wana uwezo wa kwenda kuhakikisha bidhaa zetu kwa maana ya mifugo yetu, mimea yetu, matunda yetu, mboga zetu na kila kitu itakwenda kukidhi mahitaji ya itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na kigugumizi cha muda mrefu cha kutokuajiri Maafisa Ugani. Sasa naiomba Serikali, kwa kuwa tumeamua kuingia kwenye itifaki hii, ni wajibu wetu kama nchi kuona umuhimu wa kwenda kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha ili tuweze kunufaika na hii itifaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni suala zima la watafiti. Bila utafiti pia bado hatutaenda kuleta tija kwenye hii itifaki. Watafiti wetu wametengwa, wametelekezwa, hawana chochote ambacho wanakifanya. Wapo tu wanaitwa watafiti, lakini kwa maana sasa ya kwenda kutekeleza na kupata tija kwenye itifaki, naomba Serikali ione namna bora ya kwenda kuwaongezea fedha za kutosha watafiti wetu ili waweze kufanya kazi nzuri itakayoleta matunda kwa Taifa letu kwa ajili ya hii itifaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema suala zima la wadhibiti ubora; na Mheshimiwa Ndakidemi amesema kwamba *TBS* imezidiwa, ni kweli. Sasa wakati Serikali inakwenda kuangalia ni namna gani ya kuanzisha chombo kingine ambacho kitakwenda kumsaidia *TBS,* naiomba Serikali iende ikaongeze nguvu ya bajeti, pamoja na wataalam na vitendea kazi *TBS* ili waweze kuifanya hii kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, kuna suala zima la elimu kwa watendaji wetu ambao wako mipakani. Pia naomba nchi wanachama tukiwemo sisi Watanzania, twende tukatoe elimu kwa watendaji wetu ambao wako mipakani ili waweze kuelewa mkataba huu ni namna gani ulivyoingia? Ni vitu gani vinavyozingatiwa? Ubora ni upi? Hii itaondoa changamoto kwa Watanzania wetu ambao watakwenda kufanya hizo biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo natamani pia kuishauri Serikali, ni kuona sasa itifaki hii inaenda kuwa ni mwarobaini wa changamoto mbalimbali zinazotokana na upungufu wa bidhaa zetu tunapokwenda kuzipeleka kwao ama zinapokuja kwetu. Tuliona miaka michache iliyopita,

miwili au mitatu, tuliteketeza vifaranga, lakini tuliona mahindi yetu yakikataliwa mpakani. Sasa kwa mujibu wa hii itifaki, iende ikatuweka wamoja na tutafute njia mbadala nzuri itakayokwenda kutusaidia kuondokana na hizi changamoto za kuwa tunaendelea kunyoosheana vidole na nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa msisitizo tu ni suala zima la sheria kwamba Wizara sasa mtuletee Muswada wa Sheria, Kanuni na Sera ili tuweze kupata kitu kitakachokwenda kutusaidia kuisimamia itifaki hii. Msipotuletea mapema, ina maana tutaidhinisha leo, *then* tutaenda kuweka makabatini kwenye *shelves* zetu, hatutaweza kufanya kitu chochote na mwisho wa siku itakuwa hakuna kitu chochote kinachokwenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye hili Azimio la kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Afya ya Wanyama na Usalama wa Chakula na mchango wangu utajikita kwenye eneo zima la usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuishauri Serikali kwenye eneo zima la usalama wa chakula kwa maana ya inasimamiwa chini ya wapi? *Good practice* ni kwamba masuala ya usalama wa chakula yanapaswa kuratibiwa chini ya Wizara ya Afya kwa sababu kimsingi maana ya usalama wa chakula ni kuona namna gani ambavyo utalinda walaji wasipate changamoto zozote zinazotokana na madhara ya chakula. Jambo hili ni jukumu la Wizara ya Afya, lakini sasa hapa kwetu tulichofanya

tumeweka jukumu la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* chini ya *TBS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali, maadam tumeamua kuridhia azimio hili, basi lazima tukatafakari upya na tufanye mabadiliko ambayo yatawezesha suala la usalama wa chakula yawe chini ya Wizara ya Afya na siyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo naipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa sababu wameimarisha usimamizi kwenye afya ya mimea chini ya *TPRI,* lakini hivi sasa *TBS* ina majukumu mengi na haiwezekani aendelee kuwa na majukumu yale yale. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza suala hili liwekwe chini ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile moja ya matakwa ya itifaki hii duniani chini ya *Well Trade Organization,* ni lazima nchi iwe ina Sheria ya Usalama wa Chakula. Tanzania bado hatuna Sheria ya Usalama wa Chakula. Kwa hiyo, napenda kusisitiza kwa Serikali, maadam tumeamua kuridhia azimio hili, basi Serikali ifanye jitihada ya haraka kutuletea Sheria ya Usalama wa Chakula ili tuendane na takwa hili la kidunia. Ndani ya nchi zetu za Afrika Mashariki, ni Kenya peke yake ambayo tayari wanayo Sheria ya Usalama wa Chakula. Kwa hiyo, kwa mantiki hiyo, sisi kuendelea kutokuwa na Sheria ya Usalama wa chakula, ina maana yako maeneo ambayo hatutaweza kunufaika ipasavyo. Kwa hiyo, nasisitiza Serikali ije na Sheria ya Usalama wa Chakula kwa maana ya *Food Safety* na siyo *Food Security*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nishauri kuhusu suala la usimamizi wa usalama wa afya ya mazao ya kilimo. Usimamizi wa afya ya mazao ya kilimo inapaswa iwe chini ya Wizara ya Kilimo na siyo *TBS*. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ione ni namna gani baada ya azimio hili litakapokuwa limeridhiwa na Bunge lako Tukufu, basi usimamizi wa masuala yote ya usalama wa afya ya mazao ya kilimo yawe chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia mara baada ya sisi kuidhinisha na kuridhia azimio hili, ni muhimu sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iweke jitihada kubwa ya kutoa elimu kwa wakulima wetu na wananchi wetu ili tuwe na uelewa wa haya matakwa na ituwezeshe kuhakikisha kwamba tutakuwa tunazalisha mazao yanayoendana na itifaki husika ili tusije tukajikuta tumeridhia hili azimio, lakini hatujajengea uwezo wakulima na wananchi waweze kuzalisha, kusafirisha, kusindika na kuhifadhi kadiri ambavyo itifaki inahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena kwamba tunahitaji kuwa na Sheria ya Usalama wa Chakula; naomba nirudie tena, tunahitaji suala la usalama wa chakula liwe chini ya Wizara ya Afya; naomba nirudie tena, tunahitaji suala la usimamizi wa afya ya mazao ya kilimo yawe chini ya Wizara ya Kilimo; na kwa kumalizia tunahitaji wananchi wetu na wakulima wetu wajengewe uwezo juu ya hii itifaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kupata fursa ya kuchangia kwenye itifaki au azimio hili la Jumuiya ya Afrika Mashariki linalohusiana na usalama wa mimea, wanyama pamoja na usalama wa chakula. Kutokana na maelezo ambayo yametolewa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri pamoja na taarifa ya Kamati, kitu ambacho nimejifunza, ni kwamba hii *SPS Measure* ina *component* mbili. *Component* ya kwanza inahusiana na *Sanitary Major* na *component* ya pili inahusiana na *Phytosanitary Measure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye *component* ya kwanza ya *sanitary major* ni kwamba msisitizo uwekwe

kwenye kuweka *measures* au maana yake ni hatua au vitu vinavyoweza kum-*protect* binadamu kutokana na maradhi yanayotokana na vyakula. Maana yake ni *measure to protect human from born disease.* Ndiyo kitu ambacho nimekisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu na ushauri wangu kwa Serikali utajikita kwenye kwenye usalama wa chakula *(food safety)* kwenye hii *component* ya kwanza ya *sanitary measure.* Ili twende sambamba na itifaki, ni kwamba lazima *measures* zetu tunazozichukua kama Taifa, moja kati ya vitu vinavyotakiwa tujitahidi ni kuhakikisha chakula tunachokila sisi na Watanzania wote kipo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja hapa za baadhi ya wachangiaji kwamba tumechelewa kwa muda wa miaka nane. Kuchelewa siyo tatizo, lakini tunapokiendea kitu, tuwe na uhakika wa asilimia mia moja kwamba tunakwenda kutekeleza itifaki ikiwa sisi ndani bado tuko salama na tutaji-*protect* kuingiza chakula kutoka nje ambacho hakiko salama na tutakuwa tuna ulinzi wa vyakula vyetu tunavyokula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu ni kwamba ili hizi *measures* zichukuliwe na zifanye kazi, mchangiaji aliyepita amezungumzia kwenye *aspect* moja ya sheria, lakini tunahitaji kuwa na sera ya usalama wa chakula *(policy)* ambayo haipo. Tukitaka tuende sambamba na wenzetu ni lazima tujitahidi tuwe na Sera ya Usalama wa Chakula. *The main and first thing* kwenye ile *component* ya *sanitary measure,* halafu sera ndiyo ifuatiwe na sheria pamoja na kanuni na miongozo itakayotufanya sisi tuwe salama zaidi kwenye vyakula vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ibara ya 11 ya itifaki hii ambayo inasema, itahusu nchi wanachama kuainisha, yaani kufanya *harmonization* sera, sheria, kanuni na *program* ili kufanikisha madhumuni ya itifaki hii, ni ibara imo ndani ya itifaki. Imesema, katika utekelezaji wa itifaki hii, ni lazima nchi wanachama kama *blocks* za Afrika Mashariki, tuwe au tume-

*harmonize* sera zetu, sheria zetu, kanuni zetu na miongozo yetu kwenye wanyama, kwenye mimea na kwenye usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna-*harmonize* vipi wakati hata hiyo sera hatuna; na sheria zetu bado ziko *scattered* zinazohusiana na usalama wa chakula? Hizi zetu za ndani, hazijawa *harmonized.* Huwezi kupata sheria moja ambayo imesimama kulinda usalama wa chakula. Usalama wa chakula upo kwenye sheria tofauti tofauti, ndogo ndogo; unakuta iko kidogo kidogo kila mahali; kwenye uvuvi kidogo, kwenye kilimo kidogo, kwenye vipodozi kidogo, lakini hatuna sheria mama ambayo inasimama kufanya *protections* ya aina ya vyakula tunavyokula. Huo ndiyo wasiwasi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama walivyosema wachangiaji, kuridhiwa kwa itifaki hii iwe ni *wake-up call* kwa Wizara na Serikali kwamba tunahitaji tuchukue hatua za haraka, tena haraka sana ili kama nchi tuwe na sera, sheria na kanuni zitakazotulinda sisi kama nchi kwanza, halafu litakaloilinda *block* yote ya Afrika Mashariki kutokana na vyakula tunavyozalisha na tunavyotumia kila siku kwenye maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu kwa ujumla. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Neema Mwandabila ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Serikali bila kuisahau Kamati kwa kutuletea Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya viwango vya afya ya mimea, usalama wa wanyama na chakula. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Njombe, hususan wakulima, *specific* wanawake,

natoa shukrani za dhati kwa kutuletea itifaki hii. Wananchi wa Njombe wamekuwa wanasafirisha sana mazao yakiwemo viazi, mahindi, parachichi na mazao mengine mengi kama mbao na kadhalika, kwenda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wananchi wa Njombe na wengine kwa kweli walikuwa wanapata changamoto za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia watu wanapeleka mahindi nchi za jirani wakifika kwa wale wanaosaga mahindi *millers* inaweza ikawa ni *maize or wheat* wanaambiwa kwamba mzigo wako una sumu kavu. Mtu amekuja na *semi-trailer* mbili hana mahali pa kula, hana mahali pa kulala, tukisingizia *aflatoxin* na mzigo unakuwa ushaingia nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili imekuwa ni changamoto ya kutosha, na baadhi ya maeneo kumekuwa na madalali, mara mzigo unapofika nje ya *boarder* madalali wanakuwa wanawasumbua wakulima wetu kwamba wacha nichukue mzigo nitakutafutia soko, wanakuwa wanakosa pesa zao kwa wakati. Kwa heshima na taadhima niipongeze Serikali kwa kweli kwa kutuletea Itifaki hii, ku-*ratify* hii *protocol* kwa sababu sasa itaokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nikienda Ibara ya 2 kwenye malengo ni pamoja na kuhamasisha biashara ya kilimo. Asilimia 60 ya Watanzania tumejikita kwenye kilimo kwa hiyo hii Itifaki iko mahali sahihi kabisa na imekuja wakati muafaka. Kwa hiyo, kupitia Itifaki hii, Ibara ya 2 pale tunaambiwa *promote trade in food and agriculture commodities.* Niombe sana sasa tuendelee kuwa na masoko ya mipakani, mipaka yetu yote ya Tanzania, nchi zote tunazopakana nazo, wilaya muhimu tuweke haya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizidi kupongeza Ibara ya 4(2)(a) kinasema katika masuala ya *plant health, harmonize the inspection and certification procedure of plant and plant product.* Yaani sasa tunakwenda kulinganisha, kufanya ukaguzi uwe unafanana. Sasa tunapoambiwa na nchi jirani kwamba hapa kuna sumu kuvu *(aflatoxin)* kwa

sababu sasa viwango vinakwenda kulingana, hakuna kudanganyana na kubabaishana kwamba akipima *TBS* ndio sasa itatambulika *certificate* yake na *Kenya Bureau of Standards (KBS);* huku kuna *TBS* kule kuna *KBS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunachukua mfano kuna kampuni mbalimbali ambao wana *counterpart* wao...

**MHE. NUSRAT S. HENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pindi Chana kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. NUSRAT S. HENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba *aflatoxin* ni sumu kuvu sio sumu kavu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pindi Chana unapokea taarifa hiyo?

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea na hoja yangu kuhusiana na suala zima la *aflatoxin* na sipingani na tafsiri kwa hiyo, tunaendelea na hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, *aflatoxin* ni jambo ambalo linaleta changamoto na mara mizigo inapokwenda tunapoambiwa kwamba kuna *aflatoxin* au aina nyingine ya *chemicals* ambayo haifai/sumu inaleta changamoto sana kwa wakulima wetu.

Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo Itifaki hii inakwenda kuboresha maana kuna watu wanyalukolo kuna namna yetu ya kutamka na watu wa maeneo mengine kila watu na namna yao, kwa hiyo, bora tutumie kiingereza ili kuweka muafaka. Kwa hiyo, nazungumzia suala zima la *aflatoxin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna maeneo ya kubadilishana *information.* Katika Ibara ya 9 inazungumzia suala zima la *sharing of information.* Tumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye masuala ya kilimo kwa mfano masuala mazima ya nzige namna gani tunakabiliana na changamoto ya nzige.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naunga mkono ni Ibara ya 11 *harmonization of policies, laws and regulations;* hili pia ni eneo ambalo muhimu sana tuka *harmonize* kwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 inazungumzia *boarder post control.* Naomba kushauri kwamba katika suala zima la *boarder post control* sasa tuhakikishe *boarder post* zote ni *one stop boarder post.* Baadhi ya maeneo bado hatuna *one stop boarder post*, kunakuwa na *boarder* mbili; mtu ana-*clear* upande wa Tanzania na nchi inayofuata. Lakini tunapokuwa na *one stop boarder post* kwanza inapunguza kupoteza muda kwa hiyo, muda haupotei na mzigo unakuwa *cleared* kwa haraka na mara mzigo ukiwa *cleared* kwa haraka, maana yake ni kwamba *time is money* anaweza kwenda kuchukua mzigo mwingine kupata kupeleka kule kunakostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni suala zima la Ibara ya 16 ambayo inatueleza wazi kwamba *this protocol shall enter into force upon ratification and deposit of instrument of ratification with the Secretary General by all the partner states.* Mara leo baada ya kuridhia na tunaunga mkono wote hapa kuridhia Itifaki hii, niombe sana tusichelewe ku-*deposit with the Secretary General wa East Africa Community. Secretary General who shall transmit certified true copies of the Protocol and Instruments of ratification to all the partner states.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono na nampongeza sana Waziri kutuletea Kamati naunga mkono na kwa kweli kwa niaba ya Wananchi wa Njombe

naunga mkono hoja ya kuridhia Itifaki hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Abdallah Ulega ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye majuzi alifanya ziara yake akapita kwenye Jimbo langu la Hai na kwa kweli ametuachia ahadi kubwa sana na kukidhi matarajio ya Wananchi wa Jimbo la Hai. Namshukuru sana na Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili naona limechelewa na limechelewa kwa nini? Kwa sababu tunalihitaji sana na sisi tuingie kwenye Soko la Dunia. Sasa ningependa nishauri mambo yafuatayo; Azimio hili litakuwa na faida kwetu kama tutafanya mambo yafuatayo;

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Ibara ile ya 5 inazungumza habari ya usalama wa nyama, mimea na chakula. Sasa kwenye eneo hili, sisi tumejiandaaje kuingia kwenye soko baada ya kusaini Mkataba huu? Nitaanza na eneo la Wanyama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, twende tukaimarishe Sera zetu hapa; tumekuwa tukiletewa wanyama kutoka nje ya nchi kuingia kwetu lakini pia tumekuwa tukipeleka wanayama wetu nje ya nchi baada ya muda wanarudi. Sisi tuna sheria gani ya kuweza kukinga na kuhakikisha hatupati *specie* mpya zinazoingizwa kwenye nchi yetu pengine zinaweza kuja kuharibu aina ya wanyama tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia Itifaki hii tunayoenda kusaini lazima na sisi tujiandae tuweke *standard,* tuweke maabara za kisasa ndani ya nchi yetu kupima

vinasaba vya wanyama wanaotoka ndani ya nchi na wanaoingia ili tujiridhishe kwamba kama ni Simba wa Tanzania ana vinasaba vya aina hii asije Simba mwingine akaja kuleta kitu cha tofauti. Kwa hiyo, tuwe na Sera ambazo zitaweza kutufungia. Kwenye eneo la mimea hali kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisimame hapa kwenye chakula. Hivi tulivyo tupo hivi kwa sababu ya chakula tunachokula. Sasa tuna usalama/sheria gani ambayo inalinda aina ya chakula tunachokula? Chakula sio tu kikiwa mezani; lazima tuangalie kuanzia namna ya kupanda, kuvuna na kukisafirisha. Hivi ukienda kwenye masoko yetu, tunayo miundombinu inayoweza kutufanya tukala chakula salama? Tunapojenga masoko yetu tunazingatia usalama wa chakula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri ili twende vizuri na tuweze kunufaika na Itifaki hii, basi tuhakikishe suala la usalama linakaa kisheria na kwenye miundombinu linazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze, ili tuweze kufanikiwa, hebu tukimbie haraka sana kwenda kurekebisha Sera yetu ya Kilimo. Sera hii ya Kilimo ifanane na uhalisia wa sasa hivi na ili tuweze kufanikiwa tuziimarishe pia zile taasisi zetu. Hii ni kwa sababu ili tuweze kuingia kwenye Soko la Dunia, wenzetu wanatazama sana usalama wa chakula ambao unatengenezwa kuanzia hatua ya awali. Tuimarishe Taasisi yetu ya Mlingano iliyopo Tanga ili iweze kufanya utafiti wa udongo; ni eneo ambalo tumelisahau. Tufanye utafiti tujue kwenye udongo huu tunaweza kupanda kitu gani ili tulime kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazame sasa kuongeza thamani ya mazao yetu. Hapa tulipo ili tuweze kufaidi hii hakuna namna unaweza kuingia kwenye Soko la Dunia kama huwezi kuongeza thamani ya mazao yetu. Ndio maana utaona sasa hivi wenzetu wa nchi za Jirani wanakuja hapa wanachukua mazao yetu, wanaenda kwenye viwanda vyao vidogo wanaita *sorting industry,* hizo *sorting industry*

ukitazama; bahati nzuri nimefanikiwa kufuatilia mazao yanayotoka pale kwetu Hai yanaenda nchi Jirani nikaenda mpaka huko kwao wanachokifanya wana vibanda tu wanaita *sorting industry.* Wanachokifanya kama ni karoti imeletwa pale wanapima karoti ukubwa huu inaitwa ni *grade one*, ukubwa huu *grade two;* hii itaenda nchi fulani, hii itabaki hapa watakula Watanzania, hili jambo tunaweza kulifanya kwetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana wakati tunasaini Mkataba huu, tukimbie haraka kuimarisha sheria na taasisi zetu ili na sisi tuweze kufaidi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningeshauri, ili tuweze kunufaika pia hebu Serikali itazame namna ya kuwa na kiwanja kimoja cha ndege ambacho kitawavutia watu kuja kununua mazao kwetu kupitia usafiri wa anga. Na kiwanja chenyewe tukitumie kile cha *Kilimanjaro Airport,* tuondoe kodi ndege zinapotua pale iwe ni *free*, kodi iwe ni bure pale ili tuwavutie kwa sababu changamoto iliyopo sasa hivi, mizigo kutoka huku Tanzania kwenda nje ya nchi ipo ya kutosha lakini mizigo ya kutoka nje ya nchi kuja huku haitoshi. Sasa ili kuwavutia watu waweze kuja kununua mazao yetu, tuweke Kiwanja cha *KIA* kile kiwe cha mkakati tuwaambie leteni ndege zenu msilipe kodi. Tukiamua hivi, itatusaidia sana kuhakikisha tunafaidi kwenye Itifaki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; niombe hebu tutazame sasa hivi. Tumeshazungumza muda mrefu Serikali yenyewe pamoja na kwamba tunafanya kwa ubia, hebu tengenezeni kiwanda kimoja cha mfano cha kuongeza thamani ya mazao yetu. Wananchi, tunaweza tukafanya kwa mfumo wa ushirika kama tunavyofanya kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa ukanda wa kaskazini pale Hai mnajenga kiwanda cha kufungasha mazao, wanaotoka Tanga wanakuja wanafungashia pale

yanaingia kwenye *cold room* ya *KIA* iliyopo pale yanaenda nje ya nchi, ili uwekezaji wa aina huu utatusaidia sana lakini kama tutasaini Mkataba huu na hatutaangalia taasisi zetu, hatujajiandaa kuingia kwenye Soko la Dunia ambalo na lenyewe lina *standard* ya bidhaa zinazotakiwa kuingia huko, tutakuwa hatujafaidi Mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri sana tuzingatie mambo haya, tuimarishe Sera yetu ya Kilimo, tuwafundishe wakulima wetu kulima kisasa, tulete sheria hizi tatu kwa maana ya wanyama, mimea na chakula tuzitengeneze hapa na tuhakikishe miundombinu yetu inakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Neema Mwandabila atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Bunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba hili jambo ni jema kwa maslahi ya Taifa letu na tunaamini sisi kama Watanzania tunakwenda kunufaika. Niwapongeze Wizara kwa kuliona hili na kulileta kwetu ili tuweze kulijadili*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niongelee sana kwenye Sera ya Chakula na Lishe. Unapoongelea chakula na lishe, ndipo ambapo utaona kwamba mimea, wanyama na usalama wa chakula unapoenda kuangukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Chakula tunayoitumia mpaka sasa ni ya mwaka 1992. Kiuhalisia

tunaona ni Sera ambayo imepitwa na wakati na inahitajika kufanyiwa marekebisho ili kuendana na wakati na mahitaji ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)* kwanza niwapongeze kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha hali ya lishe ya Watanzania inaendelea kuwa vizuri. *TFNC* walianza zoezi la mapitioa ya Sera ya Lishe mwaka 2015/2016 na kimsingi mwaka 2017 waliweza kutoa Waraka ambao waliuwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri ambao sekretarieti na Bunge zilipitia zikaona ipo haja ya kuwa na Sera ya Chakula na Lishe. Mpaka sasa hivi Sera ya Chakula na Lishe bado haijapitishwa kwa marekebisho ambayo yalikuwa yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tunachofahamu mpaka sasa hivi kama Taifa tunazo Kamati za Lishe ambazo zimekuwa zikiendelea kufanya kazi na Kamati ya Lishe hii ni mtambuka. Hapa najaribu kuonesha ni kwa nini tunahitaji Sera ya Chakula na Lishe. Unapoongelea lishe ni kitu mtambuka kinagusa idara nyingi. Kitu ambacho huwezi ukaongelea usalama wa chakula peke yake bila kuiweka kwenye Sera ya Chakula na Lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitamani tunapokuwa tunaenda kukimbizana na hili Azimio tukumbuke kwamba katika nchi yetu kuna baadhi ya mambo ambayo hayajakaa vizuri ikiwamo na Sera ya Chakula na Lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, tunafahamu kwamba usalama wa chakula umekuwa ukiathiri lishe za wananchi wetu na masuala ya usalama wa chakula yanagusa mambo ya kuanzia ngazi ya uzalishaji kwenye kilimo kwa maana unapolima lakini pale unapoenda kwenye usindikaji wa hivi vyakula lakini pia utakuta wakati wa *transportation,* usafirishaji wa haya mazao na hawa wanyama na pia katika eneo la matumizi yaani uhifadhi wa hivi vyakula. *(Makofi)*

Nheshimiwa Naibu Spika, na ninapokuwa nasema haya, nilitamani wasizingatie suala moja tu la sumu kuvu,

wakumbuke kwamba kuna maeneo mengine ambayo mfano kuna maeneo ambayo yanakuwa na *heavy metals* mfano maeneo yenye zebaki. Kwa hiyo, tunapokuwa tunatengeneza maabara zetu zizingatie vitu vyote ambavyo vitakuwa na athari ya vyakula vinavyoingia nchini mwetu lakini hata vyakula ambavyo sisi tunatakiwa tuvitoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu waliosema ipo haja ya kuwa na maabara za kisasa kwa maana ya kwamba wananchi wetu wasipate hasara ya kusafirisha mizigo ambayo inaenda kukataliwa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu ninaiomba Serikali kupitia kikao hiki iweze kuona haja ya kuanzisha chakula na hata wanapoileta hiyo Sera ya Chakula, kwa miaka hii ambayo imekaa naona ipo bado haja ya kufanya *amendment* tena kwa sababu kuna mabadiliko ambayo yametokea hapa kati ndani ya miaka mitatu/minne hii ambayo yatakuwa hayamo mle kwenye ile sera. Kwa hiyo, badala ya kuendelea pale walipokuwa wameishia, wairudishe nyuma kidogo, hivi vitu vidogo vidogo viweze kuwa *amended* ili iendelee na mchakato, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Ulega atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii uliyonipa na pia vilevile naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hoja na hali kadhalika kuipongeza sana Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya kipekee sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri

mwenzangu na wataalam wetu kwa kazi hii kubwa walioifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tatu; nimefurahi sana juu ya michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge iliyotoa msisitizo namna ambavyo tutatakiwa tufanye sisi katika Serikali katika kuhakikisha kwamba Itifaki hii tunaitendea haki na kusogeza mbele maendeleo ya sekta mbalimbali zilizotajwa hapa katika kilimo, mifugo na uvuvi vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mifugo kwa maana ya afya ya mifugo na uvuvi, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge juu ya Serikali tulivyojipanga. La kwanza, niwatoe hofu kwenye upande wa *instrument* kwa maana ya sheria upande wa mifugo sheria zipo na tuna *competent authority* ambayo ni *Directorate of Veterinary Service.* Hii inatambulika Kimataifa Sheria ya Mifugo Duniani inamtambua yule *DVS* wetu hapa, anatambulika kabisa kwa mujibu wa taratibu zote za kidunia, Shirika la Afya ya Mifugo Duniani *(OIE)* linamtambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya Usalama wa Mifugo kwa maana ya wanyama na chakula cha mifugo ipo siku nyingi sana ni Sheria Na. 17 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2007 vilevile tukaiboresha 2019 na tuliiboresha tena mwaka 2020 ili iweze kuendana na hitaji la soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na Sheria hii ya Afya ya Wanyama, pia tunazo Sheria za *Veterinary* ambayo tuna Bodi yake na ipo kwa mujibu wa Sheria Na. 16 ya Mwaka 2003 vilevile na Kanuni zake. Vilevile tunayosheria ya Wakala wa Maabara ya *Veterinary* na yenyewe yote hii ni katika kuangalia afya ya wanyama. Sheria Sura Na. 245 ni ya siku nyingi na yenyewe pia vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwa upande wa namna tulivyo tupo vizuri kwa maana ya sheria inayolinda afya ya wanyama kwa maana ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuona namna tulivyokwenda vizuri hapa tazama tuna kitengo kwenye eneo hili la afya ya Wanyama, ndio maana katika miaka mitano iliyopita tumefanikiwa kuanzisha na kuzalisha chanjo ambazo hazikuwepo huko nyuma, yote hii ni katika lile lengo la kuhakikisha mifugo yetu inakuwa na afya njema na kuwalinda walaji wetu. Mwanzo tulianza na chanjo mbili; Chanjo ya Mdondo na Chanjo ya Kimeta, hivi leo tumeshafanikiwa kufika katika chanjo saba; tuna Mdondo, tuna Kimeta, tuna Chambavu, tuna ya kutupa mimba, vilevile tuna chanjo ya mapafu ya ng'ombe, tuna chanjo ya mapafu mbuzi na sasa tunakwenda katika chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na chanjo ya Kondoo, tukimaliza hiyo tunatengeneza ya Kichaa cha Mbwa. Hizi zote zinahusiano wa moja kwa moja wa mwanadamu na wanyama. Kwa hiyo, akiumwa mnyama na mwanadamu pia vilevile anadhurika, hiyo ni kwa upande wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, nataka niwahakikishie na ndiyo maana hata *rate* yetu ya kulinda mifugo yetu imeongezeka. Mwaka 2018/2019 tuliweka bajeti ya lita 8,000 ya kuogeshea mifugo tukaanzisha ile programu ambayo haikuwepo kwa miaka mingi sana, mwaka 2019/2020 tukaongeza kutoka 8,000 tukaenda 12,000, mwaka 2021 tumeongeza tena kutoka 12,000 mpaka 15,000 *liters* na mwaka 2021/2022 sasa tunakwenda katika lita 17,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yetu hapa ni kuangamiza kabisa ugonjwa unaosababishwa na mbung'o. Kwa hivyo, yale magonjwa yote yanayosababishwa na mbung'o yaondoke na *rate* yetu ya kupunguza maradhi haya ni kubwa sana. Tumeshakwenda chini ya asilimia 30 hivi sasa tulichobaki nacho. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge unaweza ukaona jitihada za makusudi za kushindana kuhakikisha tunalinda afya ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi kwa jitihada hizo tulizozifanya pia pamoja na kuchelewa huku kumetupa nafasi ya kujipanga vema, hapa miaka michache iliyopita hatukuwa hata na viwanda vya kuchakata nyama,

hatukuwa na viwanda vya kusindika maziwa. Nimemsikia Mheshimiwa Kiswaga hapa akitaja kiwanda cha *ASAS* ni moja katika mifano mizuri tuliyonayo. *ASAS* wana sindika maziwa na yanaweza kuuzwa kokote pale duniani, ni vile tu kwamba hizi itifaki ndiyo zimetucheleweshа, lakini niseme kwamba maziwa yao ni mazuri ukiingia leo katika baadhi ya ndege za Kimataifa kama *South African Airways* unakuta mtindi wa *ASAS* unaliwa mle.

Kwa hiyo, hii yote ni mipango mizuri tunajipanga katika kujitosheleza wenyewe ndani ya nchi na vilevile kuuza njeya nchi ndiyo maana tuna *ASAS* tuna Tanga *Fresh*, tuna Kilimanjaro *Diaries* na wengineo na viwanda vya kuchakata nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha tunajitosheleza ndani, lakini tunauza na nje ndiyo maana tumefungua masoko kama yale ya Uarabuni tumemuona *Prince Crown* wa Saudia alipokuja hapa na wamepita katika machinjio zetu kadhaa. Zile machinjio wameziangalia ubora wake. Nataka niwahakikishie kwamba wameridhika sana, wamekwenda *Tan Choice* - pale Soga wameona, vilevile wamekwenda na Elia *foods* kule Namanga wameona kazi ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa samaki tunayo maabara kubwa na nzuri ya Nyegezi, ile maabara ya Nyegezi ni maabara ya Kimataifa nataka niwahakikishie inapima vimelea vya kibailojia, lakini inapima na vimelea vya kikemikali. Imekubalika Kimataifa na ndiyo maana Samaki wetu wanaweza kuuzwa Ulaya, wanauzwa Asia, wanauzwa kokote pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge maoni yenu ya namna ya kuweza kuboresha tumeyazingatia na ndiyo maana hata katika bajeti hii mialo kadhaa itatengenezwa, pamoja na kulinda afya za walaji wa ndani na kuendelea kulinda soko letu la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii nami naendelea kuunga mkono hoja azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa nafasi, lakini pili nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge waliotoa maoni, mengi ni ushauri ambao kama Wizara tutahakikisha tunauzingatia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie kwa ufupi sana. Kwanza sisi tunazalisha *locally* tuna *trade globally* kwa hiyo lazima zitakuwepo *threat* na tunai-*consider threat* waliyoitoa Waheshimiwa Wabunge hasa athari ya hofu ya suala la *GMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie kwamba mwaka jana tumepitisha sheria ndani ya Bunge lako Tukufu *(The Plant Health Act, 2020)* iliyopitishwa na ukisoma katika *definition* imesema wazi kabisa hii ni *instrument* moja tutakayoitumia ku-*control* vihatarishi vyote vya teknolojia za *GMO.* Imesema *a plant means any living plant all the parts thereof, including seeds and gem plus.* Sasa hivi ndiyo tunatengeneza Kanuni na mapendekezo ya Kamati tutaya-*consider* kwa kiwango kikubwa sana kuhakikisha kwamba tunaitumia sheria hii na mamlaka hii kuwa ni *instrument* muhimu ya *control. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninataka tu niseme kwamba Tanzania *Plant Health Authority* inatujengea uwezo mkubwa wa kuwa na maabara zetu ambazo zitakuwa *Internationally Certified* ambazo mazao yote ya kilimo yanayotoka nje ya mipaka yetu yakipata hati ya uthibitisho kutoka katika maabara zetu hizi itakuwa ni moja kwa moja tunaweza kuingia katika soko la Kimataifa. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo nilitaka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ni hoja ya Sera ya Kilimo, tuwahakikishie kwamba tutaihuisha iweze kuendana na mahitaji ambayo ni ya sasa na kuweza ku-*accommodate* mahitaji yote ya *protocol* hii. *Protocol* hii inazungumzia suala la *harmonization*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *protocol* hii pamoja na kuwa tunaipitisha leo suala la *harmonization* mnapoenda kwenye meza kama ninyi hamna *instrument* ambazo zitawafanya m-*harmonize* na wenzenu hamuwezi ku-*harmonize* chochote utakuwa *out of the game.*

Kwa hiyo, kwa kuipitisha leo *protocol* na sisi kwenda kuhuisha Sera yetu ya Kilimo na uwepo wa hii sheria ambayo imepitishwa na Bunge lako Tukufu na uanzishwaji wa hizi maabara itatujengea uwezo mkubwa wa ku-*compete* na wenzetu katika soko la Jumuiya Afrika Mashariki, lakini vilevile soko la Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja wamesema Waheshimiwa Wabunge kuhusu maabara ambazo zipo katika baadhi ya maeneo yaani isiwe kwamba *center* ya maabara ni moja. Labda tuseme Nyanda za Juu Kusini tuna maabara yetu ya *treat* ambayo ni ya chai kama Wizara, tumeanza kuiwezesha maabara ile ili iweze kuhudumia na mazao mengine ambayo siyo *specifically* ya chai mfano, parachichi na mahindi. Maabara zetu za Uyole na maabara zingine tutazijengea *capacity* ili ziweze ku-*meet* mahitaji yanayotukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kama Wizara tunajua *threat* zinazotukabili katika *protocol* hii, lakini tunazo *mitigation solution* ambazo tunaweza kupambana nazo na tutakuwa salama huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Professor* Adolf Mkenda Waziri wa Kilimo na mtoa hoja uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitazungumza kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani sana kwa Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa sababu wakati wa kuwasilisha kwa kweli walitukalisha chini kweli kweli, walichambua Itifaki kwa undani kweli kweli, waliuliza maswali mengi sana, walitaka tuwahakikishie kila kitu na maslahi ya nchi yetu yapo wapi, tunashukuru tulielewana nasi kwa upande wetu tunachukua ushauri wao wote nita- *highlight* baadhi ya vitu ambavyo wamevizungumza hapa. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu zangu za haraka haraka tumekuwa na wachangiaji 16 na wote wameunga mkono hoja na wametoa ushauri ambao ni muhimu sana kwetu kuuchukua. Sasa niweke kwa muhtasari mambo makubwa nitajaribu ku- *highlight* vitu vichache sidhani kama nitahitaji muda wote ambao umewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama kila mtu alivyosema Itifaki hii ni muhimu sana kwetu. Kwanza kwa sababu inatuwezesha sisi kufanya biashara, kuuza nje hapa tunazungumza changamoto ya soko, changamoto kubwa ya soko la mahindi, changamoto kubwa ya soko la mchele na tunazungumzia mboga mboga, na tuliona hapa karibuni tatizo la watu kutoa tafsiri kuhusu usalama wa mahindi yetu. Kuwa na itifaki kama hii kama walivyosema baadhi ya Wabunge, ambayo inatupa vigezo ambavyo vinapimika na vya uwazi za kuhakikisha kwamba hatudanganyani kama nia ya kuzuia biashara yetu isifanyike kutatusaidia sisi kuendelea kutumia soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika na nadhani wamezungumza baadhi ya Wabunge hapa, sisi ndiyo wauzaji wakubwa wa mazao ya chakula katika Jumuiya ya Afrika

Mashariki. Kwa hiyo, sisi kwa hakika ndiyo tunastahili zaidi kuisimamia Itifaki hii ili uweze kuwa na mafanikio kwa hiyo hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; hii Itifaki nayo inatuhakikishia usalama wa vile vinavyoingia hapa nchini kwetu, kwa sababu ni vigezo vya kuhakikisha usalama wa vitu vinavyoingia. Kwa hiyo, kwa kusaini hivi na kudhibiti kwamba nchi jirani kwenye Jumuiya hii haziingizi vitu ambavyo vikivuka kwanye mpaka vinakuja kuumiza afya ya watu wetu, tunakuwa tunajilinda na tunalinda watu wetu, kwa hiyo ni Itifaki ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na Itifaki hii inatukumbusha kuendelea kuboresha ubora na usalama wa bidhaa zetu kwa sababu bado tunahitaji masoko ya Ulaya, na kote kuna *SPS*, kinachozuia sana kuingia masoko ya Ulaya Marekani kwa sababu viwango vyao viko juu sana, walau tunajiwekea viwango sasa hivi vya kwenda mbele na kuhakikisha kwamba baadaye tunaweza tukaongeza ubora wetu na kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa na la muhumu ni kwamba tayari Tanzania ni *signatory* ni *member* wa *WTO*, na Itifaki ya namna ipo katika *agreement* ambazo tunazo kwenye *WTO. WTO* ndiyo inasema nchi mkiwa pamoja na mazingira yanayofanana mnaweza mka- *customize na ku-localize agreement* ambayo tayari iko *WTO*. Kwa hiyo, hata kama tusinge saini Itifaki hii bado tunabanwa na itifaki *WTO* ambayo sisi ni *member*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya sasa ni kuhakikisha kwamba tunazungumza na wenzetu, kwa mfano tu, kwenye Itifaki inasema lazima tubadilishane taarifa kwamba ni taasisi gani huko Tanzania itakuwa inahakiki usalama na taasisi gani ya Kenya, taasisi gani ya Uganda, na kadhalika. Kwa hiyo, hata mfanyabiashara anakuwa na uhakika nasi tunakuwa na uhakika unapotaka kuuza bidhaa zako katika nchi hizo unapitia upande gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Itifaki imechukua miaka minane na sehemu mojawapo ni kwa sababu kulikuwa na mjadala mrefu na kila mtu na kila taasisi imetaka kujihakikishia na baada ya pale ikaonekana umuhimu wa kutunga sheria ambayo ilitungwa mwaka jana ya afya ya mimea kuhakikisha baadaye tutakaporidhia hii tutakuwa tumeajiandaa vizuri. Sisi kwa upande wa kilimo tunaita, sheria ambayo tulitunga mwaka jana ambayo inaitwa *Plant Health No.* 4, 2020 ambayo imeanzisha taasisi inaitwa *Tanzania Plant Health and Pesticides Authority (TPHPA),* ambayo ni Taasisi muhimu kwa ajili ya shughuli za *SPS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa upande wa Mifugo na Uvuvi tayari walikuwa na sheria nyingi ambazo ametueleza Naibu Waziri hapa kwa ajili ya shughuli hizo hizo. Kwa hiyo, baada ya kuchukua miaka minane sasa hivi tunajua kabisa tumejiandaa vizuri sana na kila taasisi na kila mdau aliyekuwa na shaka ana uhakika kwamba tumezingatia maslahi na msimamo wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa na Kamati yetu ni kwamba lazima tujenge uwezo na ni kweli, wa maabara yetu na kuongeza uwezo wa kupima kwa haraka, tunakubali. Jambo kubwa ambalo pengine baadhi ya watu wanalitilia shaka ni juu ya suala la *GMO*, humu ndani Itifaki haisemi kwamba tutaruhusu bidhaa za *GMO*, kilichosemwa ni kwamba tutakaa chini na kuweka utaratibu na sheria na masimamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu *GMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna msimamo wetu na tunapokwenda kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki hakuna kinachopita bila kukubaliana wote. Tanzania hatuna sababu na hatuna nia ya kutetereka kuhusu msimamo wetu wa *GMO*.

Kwa hiyo, tutakapokaa mezani kuweka msimamo, msimamo wa Tanzania lazima tuhakikishe kwamba ndiyo msimamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ni kuwa kulikuwa na wasiwasi baadhi ya watu walihisi kwamba kwa sababu ukisoma inasema hii ni kwa ajili ya kutujengea mkakati wa pamoja ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao vilevile utatuongoza sisi kushughulika na Jumuiya nyingine, baadhi ya watu wakadhani kwamba maana yake kwamba ni kushughulika na *EPA*. Ukweli ni kwamba unapokuwa na *Trade Block*, mnapokubaliana taratibu zenu, zile taratibu zinatumika vilevile ninyi kufanya biashara na nchi nyingine na *blocks* nyingine bila kujali *EPA*. Kwa hiyo, watu walikuwa na wasiwasi kwamba ni *EPA* lakini siyo kabisa haina uhusiano wa namna yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vyovyote vile *standard* za *SPS* za Ulaya ni kubwa kweli ndiyo maana tunapata shida sana kuuza vyakula vyetu katika Jumuiya ile ya Ulaya. Kwa hiyo ingekuwa tunafanya hivyo kwa sababu ya *EPA* hizi *standard* wala sisi wengine tusingeziweza katika nchi za *East Africa Community.* Kwa hiyo, watu wengi wameliona hilo, taasisi mbalimbali zimeona na zimeridhika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo tumeambiwa hapa kwenye kujenga uwezo tunakubali sana, mimi nadhani yote tu kwa sababu *discussion* yote ilikuwa ni *positive*. Kwa hiyo, ninapenda kuchukua muda huu kutoa shukrani nyingi sana kwa Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, ametuongoza vizuri sana, na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Almas Maige na Wajumbe wote wa Kamati, kwa sababu *product* hii ni pamoja na mchujo na majibizano na *scrutiny* niliyofanya na Kamati na ninashukuru wamekuwa wa kwanza kuanza kuelezea msimamo wa Serikali, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Sasa kwa taratibu zetu nitawahoji, Wabunge wanaoafiki Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula *(The East African Community Protocol on Sanitary and Phytosanitary (SPS) Measures*).

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo na Wizara zote ambazo wameshirikiana pamoja ikiwa ni pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kwa kweli mmefanya jambo la busara kabisa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamekwisha kueleza kulileta Azimo hili wakati huu na tunaamini maadamu mlikaa muda wote huo mkichakata basi sasa mko tayari kwa ajili ya kukimbia na siyo kutembea baada ya Bunge kuridhia Azimio hili. Baada ya pongezi hizo tunawatakia kila kheri katika kuhakikisha Azimio hili linatekelezwa ili zile faida zote ambazo mmezitaja Tanzania tuweze kufaidika nazo pia.

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru sana Kamati yetu ya Kilimo Mifugo na Maji kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Azimio hili, wao wametusaidia sana kwa sababu taarifa waliyoileta hapa imeturahisishia kulielewa Azimio wote ambao siyo wanakamati wa Kamati hiyo, tunawapongeza kwa kazi nzuri na tunawashukuru kwa niaba yetu sisi sote mmefanya kazi nzuri. Pia Waheshimiwa Wabunge wote mliopata fursa ya kuchangia mmetoa mawazo ambao kama mmemsikia Waziri hapa ameyachukua mawazo yenu yote na hata zile hofu zenu mlizozieleza pia wao wamezisikia na bila shaka watazipa kipaumbele wakati wa utekelezaji wa Azimio hili, tunawashukuru Wabunge wote ambao mlipata fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijahairisha Shughuli za Bunge nadhani wakati nahoji kuna Mbunge mahali pengine watu wamesahau inawabidi tuwe tunawakumbusha kila wakati, wakati wa kuhoji usiwashe *microphone* yako kwa sababu tunavyohoji Taarifa Rasmi za Bunge zinazisikia hizi sauti, kwa hiyo wanaweka pale.

Sasa ukiwasha *mic* inaonekana ni mtu mmoja ndiyo aliyesema ndiyo kwa sababu ya kwako inakuwa inaziba sauti za watu wengine wote, tafadhali sana Waheshimiwa Wabunge tusiwashe *microphone* wakati wa kuhojiwa kwa sababu sauti inaingia kana kwamba Mbunge mmoja ndiye aliyesema ndiyo wakati ni Bunge zima mmesema ndiyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Nane kamili mchana.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 9 Septemba, 2021 Saa Nane Mchana)*